Katika tukio kama hilo, kwa kawaida, wazalishaji ni wanawake tu, wanaume hawashughuliki kamwe. Ila mume anapaswa kuwa karibu ili aweze kutumiwa katika shughuli fulani. Wanawake wazalishaji ni wale wazito (abanyago) tu, yaani watu wazima wenye uzoefu wa kutosha (Charsely, 1969 & Millet, 1992). Inawezekana hata mama wa makamo anaombwa kuwapo. Inaposhindikana kuwapata wanaostahili, wanawake wa kawaida wanaweza kusaidia. Kulingana na imani za jamii hiyo, matatizo katika kujifungua yanaweza kujitokeza kwa sababu mbalimbali.

Baadhi yake huamini kuwa ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu (*Kyala*). Hayo hayawezi kuondolewa. Mengine yanaaminika kuwa yanaweza kutokana na laana iliyotumwa na mwenye wivu, kulogwa ama kuzini sirini.

Hali ya kujifungua inakabiliwa na matatizo mengi. Baadhi yake yaliyotajwa kama hayana uhusiano na mjamzito, basi mwaguzi akimtaja mtu fulani kuwa amesababisha, mtu huyo anaitwa kujieleza. Pia, anayo nafasi ya kukana madai ya mwaguzi au labda atakumbuka ugomvi uliokuwapo kati yake na yule mwanamke. Itabidi athibitise kwa kutamka kuwa hajamloga mwanamke mjamzito. Uzazi ukiendelea kuwa mgumu, wazalishaji wanamwambia mwanaume kwa msemo usemao: ‘*Umpiki gwabhundu gukututamy*’ (Mti wa ubinadamu unatuhangaisha). Mti wa ubinadamu wakimaanisha kuwa mwanamke bado hajajifungua. Akijifungua, watu humpa mzazi hongera. Wanawake walio na watoto ndio peke yao walio na ruhusa kumtembelea mwanamke aliyejifungua. Kwa kawaida huleta zawadi mbalimbali, vikiwamo vyakula na kuni.

Aidha, kama uzazi ulikuwa mgumu, husema; ‘Tunafurahi pamoja nawe kwa kuwa umepona moto/fimbo ama mawe (mapacha). Pia, husema: ‘*Ndaga Kyala, akwimile*’ (Tumefurahi pamoja nawe kwa kuwa Mungu alikuwapo). Uzazi kama huo ndio unaowafanya na kusababisha wanaufeministi wa kiradikali kuisitiza kuwapo kwa mfumo huru wa uzazi katika jamii (Shante, 1992 & Bond, 2000). Mfumo huu hutaka watoto wazaliwe kwa kutumia mbinu za kisayansi, kwamba, mwanaume aweke mbegu zake katika chupa ili zirutubishwe, hatimaye mtoto aumbike. Pia, wanapendekeza mwanamke ajifungue kwa kufanyiwa upasuaji. Hali hii itawaepusha wanawake katika matatizo na vifo vya uzazi.

Pia, ipo misemo inayolenga kumtakia heri na baraka mtoto aliyezaliwa ili aendelee kukua vizuri kimwili na kiakili. Kulingana na desturi za jamii ya Wanyakyusa, mtoto akizaliwa, wajibu wa baba ni kuwajulisha watu wa ukoo wake, hasa wakwe (Egert, 1970). Kwa kawaida, hutumwa

kijana kuwapelekea kuku (tetea) kama mtoto ni wa kike au jogoo kama ni wa kiume. Kijana akifika (akishika kuku mkononi) anasalimu kwa kusema; ‘Mizimu wamekusaidia’. Ndipo babu wa mtoto aliyezaliwa anaweza kujibu kwa msemu huu: ‘*Ngimba, tata. Isile. Nabilaga abakikulu. Alyege itolo ifilombe fyake*’ (Kumbe, baba. Tayari amefika. Niliogopa kwa ajili ya mwanamke. Sasa aendelee kula mahindi yake). Msemu huo humtakia baraka njema mtoto aliyezaliwa.

Kwa kawaida, mtoto akizaliwa, baba mzazi anatakiwa kupumzika mpaka kitovu cha mtoto kiwe kimeanguka (Mackenzie, 1925). Lakini kama ipo kazi ya muhimu sana anaweza kuomba ruhusa kwa mtoto kupitia kwa mwanamke mzito anayejua mila na desturi za jamii. Kama baba amelazimika kwenda kulima, anashika jembe na kuchimba kidogo nje ya nyumba yake na kurusha udongo juu ya nyumba. Unyago naye anammimonia mtoto mchanga udongo kidogo juu ya kitovu akisema, ‘Baba yako amekwenda kulima.’ Hii ni baadhi ya miiko inayofungamana na mila na desturi za jamii inayohusika. Kufanya hivyo ni kutambua kikamilifu kuwapo kwa mtoto mchanga katika maskani yake anayehitaji uangalizi mahususi katika siku zake za kwanza.

Mama mzazi hawezi kutoka kabla kitovu hakijakatika. Kimila, kitovu kinalindwa kabla ya kukatika. Inasemekana kwamba, kikikatika na kuangukia kati ya miguu ya mama au ya mtoto mwenyewe, jambo hilo linafichwa ili mtoto asije akapata shida wakati wa kuoa au kuolewa, kwa sababu anaweza kuwa tasa (Hamilton, 1912). Aidha, kuna maandalizi mbalimbali kuhusiana na kutoka kwa mama. Maandalizi yakiisha, mume na mke wanakaribishwa wale pamoja, mara nyingi hufanyika kwa mtoto wa kwanza tu. Wanawake wazee wanaweza kumwambia mama mtoto, ‘Pole sana! Uliomba kumpata mgeni mchanga, sasa yupo huyo mchanga ambaye tulikuwa hatujamfahamu bado. Msemu huu ikiwa mtoto mchanga ni msichana: ‘*Isaga, juba! Mbusukulu mommbuhesya fijo*’ (Karibu, mama! Usangu ni ugenini kabisa). Pia, husema: ‘Hujambo, wewe Sangu mdogo? Yaani, karibu! Umekuja ugenini ambako

utamaduni wake ni tofauti kabisa na wa huko ulikotoka. Msemo huo hulenga kumkaribisha mtoto aliyezaliwa. Mama hushukuru kwa kusema, ‘Asante, Mungu amesaidia.’

Aidha, kama mtoto amezaliwa wakati mwezi hauonekani angani, mama anapaswa kumuonesha mtoto mwezi ukionekana tena. Vigelegele hupigwa na kusema; ‘Mwenzio yule’ kwa sababu mwezi nao ni kama umezaliwa upya. Halafu mama anauambia mwezi; ‘Tumepata mchanga mpya.’ Baada ya utambulisho huo, mama humsafisha mtoto pua na kurusha kamasi kuelekeza mwezini akisema, ‘Nimekupa, angalia asipate mafua’. Hii ni kwa sababu wakati wa mwezi mchanga huwa na mafua mengi katika jamii hiyo. Baadhi ya wanawake huurushia mwezi kipande cha mkaa kwa imani hiyo hiyo. Kulingana (1985), magonjwa ya watoto yanatibiwa kwa kufuata ushauri wa waaguzi wa kimila waliopo katika jamii hiyo Kalinga.

Mwanamke katika Misemo Inayohusu Kujifungua

Kulingana na mila na desturi za jamii hii ya Wanyakyusa, suala la kujifungua lina desturi na miiko yake. Kwa mfano, inasemekana kwamba, ikiwa mwanamke mwenye mimba alimpiga mbwa aliyekuwa na mimba au alikanyaga kipande cha ubao wa damu bila kuona matatizo yanatokea wakati wa kujifungua (Aswile, 2007). Kama alimpiga mbwa mwenye mimba, asirudie kufanya hivyo. Kama alikanyaga kipande cha ubao wa damu, mkusanyaji wa vibao huitwa ili kusaidia. Kama amelogwa, anapaswa kulogelewa kwa mganga. Mume wa mwanamke aliye na shida humwomba mganga kwa msemo huu: ‘*Unguma umbepo unkota. Unsanusye unkasi gwangu*’ (Naomba unipe dawa. Umgeuze mke wangu). Msemo huo umebeba maudhui mbalimbali kimila na kiutamaduni. Mojawapo ni kwamba, mwanamke huyo anashindwa kubeba mimba au watoto wanakufa mara tu baada ya kuzaliwa. Dawa inatakiwa ili apate mimba na watoto wasiendelee kufa kabla na baada ya kujifungua.

Mtoto aliyezaliwa kabla ya wakati au aliyezaliwa hali amekufa huzikwa kimya kimya bila kilio. Kimila, huzikwa upenuni kwa kuwa alikuwa hajaingia katika maisha ya hapa duniani, hawezi kuagwa katika maisha hayo. Mwanamke hufarijiwa kwa msemu usemao: ‘*Ndaga fijho, Kyala akwisile*’ (Pole sana, Mungu amekujia). Mwanamke aliyefiwa hujibu: ‘*Ena, Kyala anganile*’ (Asante, Mungu amenipenda). Misemo hiyo humanisha kuwa hayo ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Misemo hiyo ni ya kawaida iwapo Mwenyezi Mungu hatazamiwi kama aliyesababisha matatizo katika uzazi huo. Kama mwanamke amefariki baada ya kujifungua, kuna kilio cha kawaida. Mtoto ambaye mama yake amekufa wakati wa kujifungua, kwa kawaida, anatumzwa na bibi mzaa mama au ndugu yake wa kike.

Kwa upande mwingine, uzazi wa mapacha ni tukio linaloogopwa sana katika jamii hiyo. Hali ya kuzaliwa kwa watoto wawili ni ya kipekee, na ni mwiko hasa. Uzazi wa mapacha hutazamiwa kama ugonjwa wa kuambukiza katika jamii; na kwamba, unaweza kusababisha magonjwa mengine mabaya kwa wanadamu na wanyama. Hatua kali zilichukuliwa ili kuondoa mkosi huo. Pia, uzazi wa kutangulia miguu au matako ni mwiko. Lakini, amri zake si kali kama za uzazi wa mapacha (Joseph, 1941). Jamii nzima hushtushwa kwa uzazi wa mapacha. Mganga wa asili huombwa achukue hatua ili kuzuia ubovu kuenea (*Ukupyua ipasa*). Mganga anasalimia kwa msemu huu: ‘*Kyala akusulukile*’ (Mungu amekushukia). Maana yake, mapenzi ya Mungu hayawezi kuzuilika. Wazazi wa mapacha na watoto wao waliweza kutengwa kwa kujengewa kibanda kidogo mpaka kipindi cha hatari ya kuambukizwa wengine iishe. Hali hii inachukua mwezi mmoja hata miezi miwili.

Aidha, kama mapacha wamezaliwa kwa chifu (*Malafyale*), ndugu zake wanaarifiwa na mganga kwa msemu huu: ‘*Malafyale alinifibhoko panyuma*’ (Chifu ana mikono mgongoni). Msemu huo unamaanisha, chifu amejaliwa mapacha. Mganga anaendelea kuwaonya ndugu wa chifu kwa msemu usemao; ‘*Munginkindilagha! Mungyoghagha!*’ (Msimpitie!

Msioge!). Msemu huo unamaanisha kwamba, wasimhatarishe chifu wala mapacha waliozaliwa kwa kushirikiana kimwili. Ndugu walitakiwa kungoja mpaka chifu atakapokuwa amefunga na kuimarishwa na mganga. Halafu mganga atakapotekeleza utaratibu, ndipo ndugu zake wote watakapoendelea na maisha yao ya kawaida. Ikiwa pacha mmoja ataugua ugonjwa wa kuhara, hata kufa, basi mmoja kati ya ndugu atakuwa alivunja katazo (Meyer, 1993). Uaguzi hufanyika. Mhusika akijulikana na kukiri kosa, atalipa ng'ombe dume kwa kumpatia baba wa mapacha. Mtuhumiwa akikana, suala linaamuliwa kwa *mwafi* (jembe huchomwa moto na kuwa jekundu) mshukiwa anaamuliwa kulikanyaga. Kama hakuhusika, hataungua (jambo hilo hufanywa kwa mwongozo wa mganga kwa dawa maalumu). Kama mshtakiwa atakanyaga na kutoungua, ugonjwa hutazamwa kuwa ni mapenzi ya Mungu. Kama ni hivyo, hakuna la kufanya.

Mwanamke katika Misemo Inayohusu Ubalehe na Uchumba

Kama msichana anaingia mwezini kwa mara ya kwanza, tukio hilo ni la maana si kwa jamaa yake tu, bali kwa jamii nzima, kwa sababu anaweza kuolewa (Wilson, 1963). Msichana anapaswa kuwaambia wazazi wake kuwa; 'Nimeingia katika utu uzima.' Msemu huo ni wa kawaida katika jamii ya Wanyakyusa ukimaanisha kuwa, msichana ameingia mwezini kwa mara ya kwanza. Ndugu na jamaa wengine wote wanaarifiwa kwa msemu huu: '*Undindwana ilambalike pakitala ikyamani amumu*' (Msichana amejilaza kwenye kitanda cha majani makavu). Taratibu hufanywa mara moja na kufuatwa na sherehe ya hadharani. Msichana anaingizwa kwenye nyumba mojawapo na kujilaza humo. Hapa wanamtembelea wavulana, wasichana na wanawake. Jioni wavulana na wasichana wanakusanyika karibu na nyumba ya mwenye ubalehe wakicheza na kuimba.

Wakati wa kulala ukifika, mwenye ubalehe analala akizingirwa na wasichana wadogo, mmoja kulia kwake na mwingine kushoto kwake (Tew, 1950). Anapewa wasichana hao wadogo wakati wote wa sherehe

yake. Vijana wengine wote wanajipanga karibu nao wakilala wawili wawili; msichana na mvulana. Kwa kawaida, wanaweza kugusana na kuchocheana, lakini wanakataliwa kushirikiana kikamilifu (Mwakasaka, 1977). Kubikiri kunaadhibiwa kwa sababu ni kumharibu msichana kabla ya ndoa. Jambo hilo hupelekwa kwa chifu ili kulishughulikia kwa utaratibu. Mvulana anaonywa na anajibu kwa msemu huu: ‘*Ngomigwe*’ (Nimepigwa). Hapo mshtakiwa anakiri kosa kulingana na miiko na desturi za jamii hiyo. Aidha, kushiriki kwa vijana katika sherehe hiyo kuna msemu usemao: ‘*Ukupanja ubhusungu*’ (Kuatamia ubalehe). Muda wa mchana msichana huwa huru kutembea au kufanya kazi. Jioni anarudi katika nyumba yake. Vijana nao wanakusanyika palepale. Sherehe hiyo inaendelea kwa mwezi mmoja hivi kabla ya kuingia hedhi ya pili. Hata hivyo, jambo hilo linaendelea kupungua kwa kasi kutokana na kuwapo kwa mwingiliano mkubwa wa utamaduni wa jamii za ndani na nje ya nchi.

Ili kumaliza sherehe pombe inahitajika. Kulingana na Hamilton (1912), kama msichana bado hajaingia hedhi ya pili, ananyolewa nywele chache tu juu ya paji la uso karibu na masikio. Lakini hedhi ikiishapita ananyolewa nywele zote. Hata wasichana na wavulana walioshiriki katika sherehe wananyoana nywele. Muda wote huo pombe hunywewa. Ndipo watu wanaondoka kwenda mtoni. Mwanamke (*unyago*) anayezielewa mila na desturi anatangulia, anafuata msichana mwenye sherehe na mwisho wanafuata washiriki wote. Wanaendelea kuimba wimbo mmoja kwa kupokezana:

Unyago: ‘*Ikyene lwe (lwi)*’

Kwaya: ‘*Ikyene lwe*’

Unyago: ‘*Ikyati sanda*’

Kwaya: ‘*Ikyati sanda*’

Kwa mujibu wa waimbaji wimbo huo una maana iliyojengwa kisanaa kwa kuzingatia mila na desturi za jamii inayohusika. Wanahisi kwamba *lwe* au *lwi* ni kifupi cha *lwisi* (mto), na kwamba, *sanda* ni kifupi cha neno ‘*busanda*’ (aina ya chura). *Lwi* humaanisha mlio wa kuku, yaani wazazi hupata kuku binti akiwa mvumilivu mpaka siku ya ndoa. *Ikyati sanda* ni mruko wa chura, humaanisha tendo la kindoa. Aidha, washiriki wanamtakia binti baraka na kujaliwa uzazi mwema katika hatua hiyo ya kuingia katika utu uzima. Wakifika mtoni, msichana anaagizwa kujitupa kwenye maji. Kisha, anasuguliwa mwili mzima kwa uangalifu. Washiriki wanaoga karibu na msichana, lakini bila utaratibu. Baada ya kuoga wanarudi kijijini.

Kihistoria, wasichana waliposwa hata kabla ya kubalehe kwao (Wilson, 1959). Uchache wa wanawake uliwafanya wanaume, vijana na wazee wajipatie wake kwa njia hiyo. Yaelezwao hapo juu, maafikiano ya ndoa yaliweza kufanyika hata kabla ya kuzaliwa kwa mtoto wa kike kwa wazazi kumweka rehani. Mara chache tu msichana alichumbiwa akiishakua. Hii ilitokea pindi baba yake hakutaka binti yake achumbiwe na kufunga ndoa mapema. Wasichana wengi wanaolazimishwa kuolewa na wachumba wasio chaguo lao, hutoroka na wanaume wanaowapenda. Wazazi wa wanaume waliotoroka nao hulazimika kulipa mahari kwa wazazi wa wasichana hao.

Pia, wapo wanaokubaliana kuoana kwa kufuata mila na desturi zao kupitia washenga. Taratibu za mahari zikikamilika, baba mkwe humpelekea mshenga habari ya kwenda kumchukua binti yake ili ampeleke kwa mume aliyemtolea mahari. Baba mkwe hufanya hivyo ili msichana asije akatazamwa na kutoroshwa na wanaume wengine. Mshenga hutumia msemu huu: ‘*Nisile nkwega ifyangu*’ (Nimekuja kuchukua vyangu). Baba hujibu: ‘*Ughwabufi alipo! Ughwe bhopagha nundindwana! Une ndini ngwafi*’ (Adui yupo! We nenda na msichana! Ng’ombe uliniletea!). Pia, hutumia msemu huu: ‘*Ughwabufi lingaisile, kukute mundu ukubhopa nutwake*’ (Adui akifika, kila mtu hukimbia na

vyake). Katika msemu huo, baba wa msichana humshukuru mshenga kwa kuwa alishatoa mahari. Kwa msingi huo, humruhusu mshenga ampeleke binti yake kwa wanaomuoa.

Mwanamke katika Misemo Inayohusu Malezi

Kwa kawaida, katika jamii ya Wanyakyusa watoto huzaliwa kila baada ya miaka miwili au mitatu (Kalinga, 1945). Ili kuhakikisha watoto wanazaliwa kwa mpango zipo dawa za asili zinazotumika kuimarisha uzazi wa mpango kwa kuzuia uzazi wa mapema. Baadhi yake ni *imikungangogholo* ambayo hufungwa kiunoni mwa mwanamke kwa utaratibu maalum, kila tendo la ndoa linapofanyika. Mtoto mwingine anapozaliwa, mkubwa hakai karibu sana na mama, bali huchoza na wenzake. Katika kucheza, watoto wanawaiga wazazi wao. Wasichana hujibebesha mahindi, maua ya migomba (*ingungwe*) kama watoto migongoni. Wavulana huvivuta vitu hivyo kwa kamba kama ng'ombe. Wasichana wanapika kwa kutumia vyungu vliyopasuliwa (*ifijho*); na wavulana wanarusha mabua kama mikuki. Pia, michezo ya ngoma iliyopo katika jamii yao huigwa na kucheza.

Kimsingi, mtoto wa kike hufunzwa na mama yake kuhusu masuala mbalimbali yaliyopo katika jamii yao. Msichana hufunzwa kuhusu wajibu wake, mila na desturi za jamii yao. Polepole wasichana hujifunza kufanya kazi mbalimbali kwa nadharia na vitendo (Mwangosi, 2016). Wasichana humwona mama anavyokoka, anavyotunza moto na anavyopika chakula. Pia, hujifunza mitindo ya kupukuchua mahindi, kuchambua maharage, kuchimba na kusafisha viazi, namna ya kutengeneza pombe za asili za jamii yao, matumizi ya kinu (*ituli*) na jiwe la kusagia (*ulwala*). Aidha, wanajifunza kuchoma na kupika vyakula mbalimbali, kutafuta kuni, pamoja na shughuli za shambani. Pia, wanaelewa namna mafuta ya asili ya kupikia na kupakaa yanavyopatikana.

Kwa kawaida, kadiri watoto wanavyoendelea kukua kimwili na kiakili, huendelea kujifunza kazi mbalimbali zilizopo katika jamii yao. Kwa upande wa mtoto wa kike ni kusiliba kuta na kutengeneza sakafu, kukata nyasi za kuelekea, usafi wa nyumba na kutoa samadi ya mifugo, kazi za shambani kama kumwaga mbegu, kupanda, kupalilia, kulima, kupika chakula, kutunza na kulea watoto, kusuka mika na kufinyanga vyungu (Bernd, 1975). Hivyo, msichana mwenye umri wa kati ya miaka 14 hadi 18 anakuwa ameandaliwa vya kutosha kuweza kutunza nyumba, watoto wadogo na majukumu ya msingi katika familia na jamii kwa ujumla.

Ndoa si mapatano ya kiuchumi tu. Kuna mambo mengi yanayoonesha hali ya kupendana, kuheshimiana na kusaidiana kati ya mume na mke (Isakwisa, 2003). Kwa mfano, vijana wakitoka kufunga ndoa wanaweza kuitana, binamu (*mfyala*), mdogo wangu (*ngwangu*), dada yangu (*ilumbu*). Watu wakiona uhusiano uliopo kati ya mvulana na msichana wanaweza kutoa misemo mbalimbali: ‘*Bali nindumbula jimojene*’ (Wana moyo mmoja), ‘*Bali nilyani limolyene ilyakijinja*’ (Wana jani moja la mgomba) au ‘*Bali nindeko jimojene*’ (Wana chungu kimoja). Misemo hiyo inahalalisha na kuitikia uhusiano thabiti unaojidhihirisha baina ya wachumba wanaohusika. Tazamio kubwa la kuo na kufunga ndoa ni kupata watoto. Kila mtoto anayezaliwa anaongeza heshima ya mama, familia, ukoo na jamii kwa ujumla. Wavulana wanatazamiwa kuwa warithi na wanaweza kuleta uzito katika jamii (Bernd, 1975). Lakini kama wavulana peke yao wanazaliwa, wazazi hawaridhiki. Wasichana wanathaminiwa sana, kwa sababu wakiolewa wanawapatia mahari, hasa ng’ombe.

Pia, kuna msemu unaotumika kama mtoto amewakasirisha wazazi wake. Kwa mfano, watu husema: ‘*Ulubhabhu lwa nyale ulu akanyile, lunnyelile*’ (Ukuni wa moto alioukanyaga, umemrukia). Pia, hutumika kama mdogo amemkasirisha mkubwa au mke amemkasirisha mume wake. Msemu huu humaanisha hatua kali za kinidhamu zilizochukuliwa kwa sababu mbalimbali za kimaadili, kiutamaduni na kisheria. Kwa

mfano, ni sikitiko kubwa kwa wazazi wote ikiwa watoto hawana adabu, wezi, mwenendo mbaya wa wavulana kuhusu wasichana, kuzungukazunguka na wasichana na kutotimiza wajibu, na kadhalika (Aswile, 2007). Mambo kama haya yanaweza kuleta ugomvi kama mojawapo ya hali hizo ikiwa mbaya sana. Wazazi wanaweza hata kumfukuza mtoto. Aidha, msemu huo hutumika iwapo kuna mashaka juu ya uaminifu wa mke au wa mume. Uzinzi ukithibitishwa, ndoa inahesabika kuwa imevunjika au kutozwa faini maalum (*ukuposola*).

Hitimisho na Mapendekezo

Makala haya yamechunguza namna mwanamke anavyotazamwa katika masuala ya uzazi na malezi katika misemo ya jamii ya Wanyakyusa. Mwanamke amebainishwa kama mhimili imara katika mfumo wa malezi bora ya familia. Aidha, ameonekana kama chombo imara cha kujengea maadili ya familia na uendelevu wa kizazi kimoja hadi kingine. Matokeo ya hali hiyo huwafanya wanaufeministi kumtazama mwanamke kwa umuhimu na unyeti wake. Hivyo, amekuwa agenda ya kudumu katika kampeni za kisiasa kwa miaka mingi.

Kwa kuwa makala haya yalichunguza namna mwanamke anavyotazamwa katika masuala ya mimba, uzazi na malezi katika misemo ya jamii ya Wanyakyusa, ni vema kama watafiti wengine watachunguza kuhusu mwanamke, desturi na miiko katika shirikina (semi), methali, nahau na vitendawili vya jamii ya Wanyakyusa. Shirikina ni vielelezo vya mabaki ya imani na itikadi zinazohusishwa na mitazamo jadi ya jamii. Aidha, ni vizuri kuchunguza nafasi ya wanawake katika tanzu zilizodokezwa ili kuchunguza falsafa kuhusu mwanamke, harakati na maendeleo yake katika jamii ya Wanyakyusa na nyinginezo hapa nchini.

Marejeleo

Abdun, N. H. (2000). *Ukombozi wa Mwanamke*. Morogoro: Mzumbe

Book Project.

Aswile, A. (2007). *An Examination of Language Use in the Bhanyakyusa Wedding Songs. A Research Report for the Requirements of the Bachelor Degree (Unpublished)*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Bader, Z. (1974). 'Social Condition of the Peasant Women in Zambia and Pemba.' Paper No, 18 Iliyowasilishwa katika Semina ya Wanawake Brulap. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Bernd, A. (1975). *The Reason for Young Marriage for the Nyakyusa and Safwa*. Dresden.

Bernd, A. (1984). *The Sense of Dower by the Nyakyusa and Safwa*. Dresden.

Bond, S. (2000). 'Culture and Feminine Leadership', In *Women Power and the Academic From Rhetoric to Reality*. New York: Berghahn Books.

Booker, M. K. (1996). *A Practical Introduction of Literary Theory and Criticism*. New York: Longman USA Publishers.

Challigha, N. E. (2011). *Usawiri wa Mwanamke na Mgawanyo wa Majukumu Kijinsia katika Fasihi Picha ya Katuni Mnato za Kiswahili. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada*

ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chamba, L. A. (2011). *Dhamira Kwenye Nyimbo za Wasanii Wasioona na Mtazamo kwa Jamii. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa)*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Charsely, S. R. (1969). *The Princes of Nyakyusa*. Nairobi.

Chodorow, N. J. (1991). *Feminism and Psychoanalytic Theory*. London: Yale University Press.

Coser, L. (1963). *Sociology Through Literature: An Introductory Reader*. Englewood.

Dworkin, A. (1981). *Ponography Men Pssessing Women*. London: London's Press.

Eggert, Y. (1970). *The Presentation of Nyakyusa on the Highest Knowledge*. Bielefeld.

Farsy, A. S. A. (1965). *Ndoa na Talaka na Maamrisho Yake*. Kutub Khan: Delhi, India.

Felluger, D. F. (1998). 'Undergraduate Introduction to Critical Theory' <http://scout.cs.wisc.edu/scout/report/socsci/> 26. 08. 2018, Saa 7: 41 Mchana.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: London Publishers House.

Guethel, A. (1981). *Sociology of Housework*. New Yor: Pantheon Books.

Hamilton, J. T. (1912). *Twenty Years of Pioneer Missions in Nyasaland*.

Bethlehem.

Isakwisa, C. (2003). Nyimbo za Harusi za Wanyakyusa na Mabadiliko ya Jamii. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Kwanza (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Joseph, B. (1941). *Giving Birth To Twins By Nyakyusa*. Hamburg.

Kajeza, T. (2016). Usawiri wa Mwanamke Katika Fasihi Andishi:

Mifano Kutoka Katika Riwaya ya *Machozi ya Damu* (200)

ya E. Shigongo. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya

Shahada ya Kwanza (Haijachapishwa). Mbeya: Chuo Kikuu cha

Tumaini Makumira.

Kalinga, O. J. M. (1985). *A History of The Ngonde Kingdom Of Malawi*. Berlin.

Kannedy, R., & Bartlett, K. (1992). *Feminist Legal Theory: Readings in Law and Gender*. New York: Columbia University Press.

Kiango, S. D. (1992). Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya za

Kiswahili za Kenya 'Baragumu', CKM) 102: 84 - 91.

Konter, J. H. (1974). *Changing Marital Relations Among the Nyakyusa, Rungwe District, Tanzania*. Leiden.

Mackenzie, D. R. (1925). *The Spirit-Ridden Konde*. London.

- Lerman, H. (1990). *Feminist Ethics in Psychotherapy*. New York: Springer Publishing Company
- Liyong, L. T. (1972). *Popular Culture in East Africa*. Nairobi: Nairobi University.
- Meyer, T. (1993). *Wa-Konde: Maisha, Mila na desturi za Wanyakyusa*. Songea: Peramiho Printing Press.
- Millet, K. (1977). *Sexual Politics*. London: Virago Press.
- Momanyi, C. (1998). Usanii wa Mwanamke wa Kiislamu katika Jamii ya Waswahili kama Iliyobainika katika Ushairi wa Kiswahili. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Momanyi, C. (2001). 'Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert' katika *Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI, uk. 53 - 65.
- Momanyi, C. (2009). 'Nadharia ya Mtazamo-Kike katika Mukstadha wa Kiafrika'. Mhadhiri Chuo Kikuu cha Kenyatta. Makala Iliyotarajiwa Kuchapishwa katika Jarida la Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mshana, R. (1996). 'Nafasi ya Wanawake katika Mageuzi ya Kisiasa na Uchumi' katika *Jarida la Kichungaji*. Juzuu 3, Na 1. Uk. 28 – 36
- Msamilah, E. M. (2012). Uainishaji wa Ngeli za Nomino katika Lugha ya Kinyakyusa Kimofolojia na Kisemantiki. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Dar es Salaam: East African Education.

- Mtandao wa Jinsia Tanzania (2001). 'Kuelekea Kwenye Usawa: Taswira ya Mwanamke Tanzania'. Dar es Salaam: SARDC.
- Mugane, D. (2012). *Nafasi ya Mwanamke katika Jamii*. USA: Harvard Univesity Press.
- Muindi, A. (1996). *Usawiri wa Wahusika Makahaba katika Vitabu vya Said Ahmed Mohamed. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa)*. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mutembei, A. K. (2005). *Kisiki Kikavu*. Dar es Salaam: E & D Limited.
- Mwabuka, M. (2013). *The Changing Roles of Banyakyusa Oral Poetry in the Contemporary Setting. A Thesis Submitted in Fulfillment of the Requerements for the Degree of a Doctor of Philosophy (Unpublished)*. Dar es Salaam: Open University of Tanzania.
- Mwabukusi, A. (2014). *Nyimbo za Kazi Katika Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Kwanza (Haijachapishwa)*. Mbeya: Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji.
- Mwakanjuki, N. (2011). *Athari za Mabadiliko ya Kijamii na Kiuchumi kwa Nyimbo za Kapote za Mwimbaji Mwandwanga katika Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa)*. Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mwakasaka, C. S. (1977). *The Oral Literature of Banyakyusa. A Research Report Submmited in Apartial Fulfilment of the Requirement for the Award of Master Degree (Unpublished)*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.
- Mwambusye, D. (2006). *A Guide to Nyakyusa Cultural Heritage*. Tukuyu: Tukuyu Highland Press.
- Mwambusye, D. (2013). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kinyakyusa*. Tukuyu: Tukyu Highland Press.

- Mwangosi, G. (2016). 'Kufungamana kwa Vitendawili vya Wanyakyusa na Matukio ya Kijamii'. Iringa: Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha, RUJASS, Vol 2: 50 – 67.
- Mwangosi, G. (2017). 'Usawiri wa Nyimbo za Magosi za Wanyakyusa katika Mukstadha wa Tanzania'. Iringa: Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha, RUJASS, Vol 3: 92 – 124.
- Narizvi, S. (1982). *The Sociology of Literature of Politics*. Australia: Edmund Burke.
- Nassoro, B. (2004). Nyimbo za Unyago za Wasagara. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Kwanza (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Njewe, D. C. (2007). Manifestation of Cultural Performances in Traditional African Films. A Research Report Submitted as a Partial Fulfilment of the Requirement of Award of Master Degree (Unpublished). Dar es Salaam: University of Dar es Salaam. (Unpublished). Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.
- Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Okeke, P. (1996). 'Post-Modern Feminist and Knowledge Productions: The African Context in Africa Today'. Vol. 43, No. 3. July September, 1996. Boulder: Lynne Rienner Publishers.
- Pullen, C. (2006). *Marxist Against Feminists on Education*. London: Routledge.
- Rosaldo, M. Z. (1974). 'Women Culture and Society: A Theoretical Overview in Michelle Zambalist' katika Rosaldo and Liuse, L. (wah) katika *Women Culture and Society*. Stanford University Press.

- Sanga, A. (2013). *Wanawake ni Injili katika Ujasiriamali*. Dar es Salaam: Ujuzi Education Publishers Limited.
- Shamte, H. (1992). *Mwanamke Katika Jamii*. Imepakuliwa 29 Oktoba 2018, katika <http://www.islamtanzania.org>.
- Shorter, A. (1969). *African Oral Tradition, History and Literature*. Columbia: Columbia University.
- Selden, R. (1990). *The Theory of Criticism*. New York: Longman.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Silbermann, A. (1963). *The Sociology of Music*. London: Routledge and Kegan Paul Limited.
- Siranchi, B. M. (1992). *Hadhi na Hali ya Mwanamke katika Riwaya za S. A. Mohamed. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa)*. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Sozigwa P. (1993). *Majukumu ya Nchi za Kusini: Ripoti ya Tume ya Kusini*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Steven, Y. (2011). *Athari za Maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Nyimbo za Watoto Waishio Mijini: Mjini Mbeya na Tukuyu. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa)*. Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Tanzania Institute of Education (2006). *East Africa From 1850 to the Present*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Tew, M. (1950). *People of the Lake Nyasa Region*. London: SAGE Publications.

Wandera, S. (1996). Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili 1800 – 1900 Uhalisi au Ukandamizwaji? Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Njoro: Chuo Kikuu cha Egerton.

Wilson, M. (1959). *Communal Rituals of the Nyakyusa. An Account of the Impact of Colonial Rule and Christian Teaching on the Nyakyusa Society and Beliefs*. London: Oxford University Press.

Wilson, M. (1963). *Good Company: A Study of Nyakyusa Age Villages*. Boston: Beacon Press.

York, J., et al. (1991). 'We are the Feminists That Women Have Warned Us About' in Gunew, S (Mh). *A Reade in Feminists Knowledge*.

Uainishaji wa Ngeli za Nomino za Lugha ya Kinyakyusa Kimofolojia Mussa E. Msamilah

Idara ya Taaluma

Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu - ADEM

E-mail: mmsamilah@gmail.com

Ikisiri

Ngeli za nomino za lugha ya Kinyakyusa zimeorodheshwa na Johnston (1919), Felberg (1996), Samwel (2008) na Lusekelo (2009). Katika machapisho hayo hakuna maelezo ya kina yanayofafanua kuhusu uainishaji wa ngeli za nomino za lugha ya Kinyakyusa. Jitihada pekee

zilizokwisha fanyika ni kuorodhesha kiambishi tangulizi (Kbt) na kiambishi ngeli (KNg) vikiambatanishwa pamoja. Hivyo, makala hii imekusudia kuainisha ngeli za nomino za lugha ya Kinyakyusa kimofolojia. Katika kuainisha ngeli hizo, makala hii inafafanua kwa kina viambishi ngeli vinavyowakilisha kila ngeli pamoja na alomofu zake. Vilevile ufafanuzi wa viambishi ngeli vinavyowakilisha kila ngeli umeambatana na mifano ya nomino ambazo zinaweza kuwakilishwa na kuwekwa katika ngeli hizo. Aidha, katika uainishaji wa ngeli hizo na ufafanuzi wake, Kbt na KNg vimetenganishwa. Wango⁶ uliolengwa katika utafiti huu ulikuwa ni wazungumzaji wa lugha ya Kinyakyusa ambao wanaishi katika halmashauri ya Busokelo, mkoani Mbeya. Data zilikusanywa katika kata za Isange, Luteba na Mpombo. Mbinu iliyotumika kupata sampuli ni nasibu tabakishi. Sampuli iliyotumika ni watafitiwa thelathini (30); kila kata watafitiwa kumi (10) wanaume watano (5) na wanawake watano (5). Data hizo zilikusanywa kwa njia za dodoso, ushiriki na mahojiano. Kwa ujumla, makala hii inahitimisha kwamba kuna ngeli kumi na mbili za nomino katika lugha ya Kinyakyusa zikiainishwa kwa kigezo cha kimofolojia.

Utangulizi

Mfumo wa ngeli ni sifa mojawapo ya kimuundo ya lugha za Kibantu ambapo nomino zinapangwa katika makundi kwa kuzingatia kigezo fulani. Kutokana na nomino za lugha za Kibantu kuwa na sifa ya mfumo wa ngeli, wataalamu kama Ashton (1944), Katamba (2003), Kihore na wenzake (2003), Kahigi (2005), Matei (2008) na Mwendamseke (2011) wamezipanga nomino za lugha za Kibantu katika makundi ambayo kitaaluma yanaitwa ngeli za nomino. Katika uainishaji wao wametumia kigezo cha kimofolojia. Makundi ya nomino yanapewa namba, utaratibu ambao uliasisiwa na Bleek (1869). Utaratibu huo umetuwezesha kujua idadi ya ngeli za nomino katika lugha mbalimbali za Kibantu.

⁶ Watu wote waliolengwa katika utafiti

Aidha, kuna mikabala mikuu miwili ya uainishaji wa ngeli za nomino kwa kutumia kigezo cha kimofolojia. Mkabala wa kwanza ni ule ambao viambishi vya umoja na wingi vinaunda ngeli tofauti. Kwa mfano, kwa kutumia mkabala huu, Polome (1976: 94 - 95) aliainisha ngeli kumi na nane za nomino za lugha ya Kiswahili; na Rugemalira (2005: 23) aliainisha ngeli kumi na nane za nomino za Kirunyambo. Katika makala hii mkabala uliotumika katika kuainisha ngeli za nomino ni ule unaoweka viambishi vya umoja na wingi, pamoja kuwakilisha ngeli moja. Utaratibu wa namba umetumika katika uainishaji wa ngeli za nomino za lugha ya Kinyakyusa ili kujua idadi yake.

Uainishaji wa ngeli za nomino unazingatia miundo ya nomino. Nomino za lugha za Kibantu zina miundo tofautitofauti. Mutaka na Tamanji (2000: 150) wanaeleza kuwa miundo ya nomino katika lugha za Kibantu inaweza kubainishwa kwa namna tatu kama vile kiambishi awali+shina (KA+Sh), kiambishi tangulizi+kiambishi awali+shina (Kbt+KA+Sh) na kiambishi awali fuatishi+kiambishi awali+shina (KAF+KA+Sh). Petzell (2008: 47) anaeleza kuwa muundo wa nomino za lugha za Kibantu kwa ujumla ni irabu tangulizi+kiambishi ngeli+shina (IT+KNg+Sh). Aidha, Mwendamseke (2011: 50) anaeleza kuwa miundo iliyoelezwa na wanaisimu Mutaka na Tamanji sio lazima ijitokeze yote katika kila lugha. Mwendamseke amengeza muundo mwingine wa kiambishi tangulizi+kiambishi awali fuatishi+kiambishi awali+shina (Kbt+KAF+KA+Sh) unaojitokeza katika nomino za Kibena.

Miundo iliyoelezwa na wanataaluma hao ni kweli inapatikana katika nomino za lugha za Kibantu, lakini ikumbukwe kuwa lugha hizo zinatofautiana na kufanana kwa namna fulani. Hivyo, miundo iliyoelezwa inaweza kutokea yote katika lugha fulani au ikatokea michache. Vilevile kuna uwezekano wa kutokea miundo tofauti kabisa na iliyoelezwa na wanataaluma hao kama alivyoeleza Mwendamseke (2011) kuwa lugha ya Kibena ina muundo wa Kbt+KAF+Sh.

Mada Iliyochunguzwa

Ngeli za nomino za lugha ya Kinyakyusa zimeorodheshwa na Johnston (1919), Felberg (1996), Samwel (2008) na Lusekelo (2009). Katika machapisho hayo hakuna maelezo ya kina yanayofafanua kuhusu uainishaji wa ngeli za nomino za lugha ya Kinyakyusa. Jitihada pekee zilizofanyika ni kuorodhesha kiambishi awali tangulizi (Kbt) na kiambishi awali ngeli (KNg). Jambo hili lilimsukuma mtafiti kufanya uchunguzi wa kina kuhusu ngeli za nomino za lugha ya Kinyakyusa. Kwa hiyo, makala hii inahusu uainishaji wa ngeli za lugha ya Kinyakyusa kimofolojia.

Mbinu na Mipaka ya Utafiti

Makala hii yameshughulikia suala la uainishaji ngeli za nomino katika lugha ya Kinyakyusa kimofolojia. Utafiti ulifanyika mkoani Mbeya katika halmashauri ya Busokelo. Data za msingi zilipatikana uwandani kwa mbinu za dodoso, ushiriki na mahojiano katika kata ya Luteba kijiji cha Ipuguso, Mpombo katika kijiji cha Lusanje na Isange katika kijiji cha Isange. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa kuwa yalikuwa na mawanda ya kutosha kukidhi mahitaji ya makala hii. Aidha, data za upili zilikusanywa maktabani kwa mbinu ya kinyaraka katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Maktaba hii iliteuliwa kwa kuwa ina data za kutosha zilizohusiana na mada ya makala hii.

Mkabala wa Uainishaji wa Ngeli za Nomino

Katika makala hii tumetumia mkabala wa Jozi ya Viambishi vya Umoja na Wingi (JVUW) uliobuniwa na wanasarufi wa Kiswahili, akiwamo Ashton (1944) kama alivyonukuliwa na Kihore na wenzake (2003: 97). Kwa kuzingatia mkabala wa JVUW, ngeli za nomino huainishwa kwa kuwakilishwa na jozi ya viambishi. Kiambishi kimoja kinakuwa cha umoja na cha pili huwa cha wingi.

Mkabala wa JVUW ulitumika katika uchunguzi wa mada yetu kwa kuitazama nomino kuwa ni moja ikiwa katika umbo la umoja na la wingi. Aidha, mkabala huo unachunguza ngeli kadhaa zinazowakilishwa na kiambishi kimoja cha nomino kwa baadhi ya ngeli (Kihore na wenzake, 2003). Kwa msingi huo, mkabala huo ulitumika kuzichunguza nomino za lugha ya Kinyakyusa zenye viambishi vinavyofanana kwenye umoja na kutofautiana kwenye wingi. Nomino za lugha ya Kinyakyusa zilichunguzwa kwa kina kwa kuwa baadhi yake zina viambishi vya umoja vinavyofanana, lakini viambishi vya wingi hutofautiana; hivyo ilikuwa rahisi nomino hizo kuwekwa katika ngeli zinazohusika.

Kwa ujumla, mkabala huu ulitumika kama msingi wa uainishaji wa ngeli za nomino katika lugha ya Kinyakyusa. Hii ni kwa sababu uainishaji wa ngeli za nomino katika lugha za Kibantu upo katika misingi ya kimofolojia (Kahigi, 2005). Pia, mkabala ulitumika kuweka viambishi vya umoja na wingi katika ngeli moja. Hali hiyo ilipunguza idadi ya viambishi kujirudiarudia kwa kuwa nomino inayoshughulikiwa kwa kiambishi cha umoja ni hiyo hiyo inapokuwa katika wingi.

Uainishaji wa Ngeli za Nomino za Lugha ya Kinyakyusa Kimofolojia

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa uwandani, nomino za lugha ya Kinyakyusa zinaonesha kuwapo kwa miundo ya aina tano. Muundo wa kwanza ni ule wa IT+KNg+Sh ambao ndio hujitokeza zaidi katika nomino hizo. Nomino zenye muundo huo zinapotumika kama jibu la swali huwa na muundo wa KNg+Sh. Kwa mfano, nomino *a+ma+fumbi* ‘mayai’ ina muundo wa IT+KNg+Sh, lakini kama ni jibu la swali huwa na muundo wa KNg+Sh. Muundo wa pili ni KNg+Sh, ilihali wa tatu ni Sh pekee, na muundo wa nne ni IT+Sh. Nomino zenye muundo wa IT+Sh ni zile ambazo hazina KNg katika umoja na wingi, bali zina IT na Sh tu. Aidha, muundo wa tano ni KNg+KNg+Sh. Huu ni muundo wa nomino za mahali fuatizi ambazo zimehamishwa kutoka katika ngeli

nyingine kwa kuambikwa KNg cha ngeli ya mahali. Muundo huu hutokea endapo nomino inayohamishwa ina KNg. Kiambishi hicho hakidondoshwi nomino inayohusika inapoambikwa kiambishi cha mahali, hivyo inakuwa na viambishi ngeli viwili. Mifano ya nomino zenye muundo huu ni *pa-ki-bhanja* ‘uwanjani’ (KNg+KNg+Sh) na *ku-ky+alo* ‘shambani’ (KNg+KNg+Sh).

Kwa muhtasari, uainishaji wa nomino za Kinyakyusa unaonesha kuwapo kwa miundo ya aina tano. Uainishaji ulizingatia kigezo cha KNg kinachoonsha nomino ikiwa katika umbo la umoja na wingi. Hivyo, kwa mujibu wa uchanganuzi wa data zilizokusanywa uwandani, zifuatazo ni ngeli za nomino za lugha ya Kinyakyusa kimofolojia.

Ngeli ya 1, mu-/bha-

Ngeli ya 1 katika lugha ya Kinyakyusa inawakilishwa na viambishi //mu-// umoja na //bha-// wingi. Kiambishi //mu-// cha umoja cha ngeli ya 1 kina alomofu sita ambazo zinatokea kutokana na michakato ya kifonolojia kama vile uyeyushaji, urefushaji, udondoshaji, unazalishaji, uchopekaji, usimilishaji na ukakaaishaji. Alomofu hizo ni {mu-}, {m-}, {mw-}, {n-}, {mo-} na {∅}. Kiambishi cha wingi cha ngeli ya 1 ni /bha-/ ambacho kina alomofu mbili ambazo ni {bha-} na {bho-}. Nomino za Kinyakyusa zinazopangwa katika ngeli hii ni kama zilizooneshwa katika mifano ifuatayo;

(i) mu-/bha-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|--------------------|----------------------|
| | u - mu - ndu ‘mtu’ | a - bha - ndu ‘watu’ |
| | IT KNg Sh | IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Kama inavyooneshwa katika mfano wa (i) katika lugha ya Kinyakyusa ni nomino moja tu inayoanza na {mu-} ya kiambishi //mu-// kinachowakilisha ngeli ya 1 umoja. Nomino nyingi zinaanza na alomofu kama vile {m-}, {mw-}, {n-}, {mo-} na {∅}. Hali hii imetokana na wazungumzaji wa lugha hiyo kurahisisha matamshi kwa sababu umbo la ndani la kiambishi hicho ni //mu-//. Mifano ya nomino hizo ni kama ifuatavyo:

(ii) m-/bha-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|--|---|
| (a) | u - m - papi 'mzazi' IT KNg Sh | a - bha - papi 'wazazi' IT KNg Sh |
| (b) | u - m - puti 'mchungaji' IT KNg Sh | a - bha - puti 'wachungaji' IT KNg Sh |
| (c) | u - m - piji 'mpishi' IT KNg Sh | a - bha - pishi 'wapishi' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (ii) kwenye umoja zinawakilishwa na {m-} ya kiambishi //mu-// kinachowakilisha ngeli ya 1 katika lugha ya Kinyakyusa. Hali hii inajitokeza pia katika lugha nyingine za Kibantu kama vile Kiswahili.

(iii) mw-/bha-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|---|--|
| (a) | u - mw - ana 'mtoto' IT KNg Sh | a - bha - ana 'watoto' IT KNg Sh |
| (b) | u - mw - ipwa 'mjomba' IT KNg Sh | a - bha - ipwa 'wajomba' IT KNg Sh |
| (c) | u - mw - anike 'mwanamke' IT KNg Sh | a - bha - anike 'wanawake' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (iii) kwenye umoja zinawakilishwa na {mw-} ya kiambishi //mu// katika lugha ya Kinyakyusa. Hali kama hiyo inajitokeza pia katika lugha ya Kiswahili kutokana na mchakato wa uyeyushaji.

(iv) mo-/bho-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|--------------------------------------|---|
| (a) | u- mo - lolo 'mpole' IT KNg Sh | a - bho - lolo 'wapole' IT KNg Sh |
| (b) | u - mo - lo 'mvivu' IT KNg Sh | a - bho - lo 'wavivu' IT KNg Sh |
| (c) | u - mo - sighwa | a - bho - sighwa 'waumini' |

| | | |
|--|-----------|-----------|
| | ‘muumini’ | IT KNg Sh |
| | IT KNg Sh | |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (iv) kwenye umoja zinawakilishwa na {mo-} ya kiambishi //mu-// na kwenye wingi zinawakilishwa na {bho-} ya kiambishi //bha-//.

(v) ø-/bha-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|---------------------------------------|---|
| (a) | ø - ø - tata ‘baba’ IT KNg Sh | a - bha - tata ‘baba’ IT KNg Sh |
| (b) | ø - ø - jhubha ‘mama’ IT KNg Sh | a - bha - jhubha ‘mama’ IT KNg - Sh |
| (c) | ø - ø - sinde ‘doto’ IT KNg Sh | a - bha - sinde ‘doto’ IT KNg - Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (v) kwenye umoja haziwakilishwi na kiambishi ngeli chochote, lakini kwenye wingi zinawakilishwa na kiambishi ngeli //bha-//. Hali kama hiyo inajitokeza pia katika lugha nyingine za Kibantu kama vile Kiswahili na Kibena.

Aidha, muundo wa nomino kuundwa na Sh peke yake hujitokeza nomino inapokuwa katika umoja, lakini ikiwa katika wingi hubadilika na kuwa na muundo wa IT+KNg+Sh kama inavyooneshwa katika (v). Muundo huu, pia huruhusu nomino za baadhi ya wanyama pori kama tumbili, mbwamwitu, nyoka na kobe kuingizwa katika ngeli hii kama inavyooneshwa katika (vi):

(vi) ø-/bha-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|---|---|
| (a) | ø - ø - kajhamba 'kobe' IT KNg Sh | a - bha - kajhamba 'kobe' IT KNg Sh |
| (b) | ø - ø - kitumbhi 'kifutu' IT KNg Sh | a - bha - kitumbhi 'vifutu' IT KNg Sh |
| (c) | ø - ø - salila 'tumbili' IT KNg Sh | a - bha - salila 'tumbili' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (vi) ni za wanyama pori na zina muundo wa Sh peke yake zikiwa kwenye umoja. Hivyo, kiambishi ngeli ni kapa, lakini kwenye wingi zinabadilika na kuwa na muundo wa IT+KNg+Sh.

(vii) n-/bha-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|------------------------------|--------------------------------|
| (a) | u - n - kikulu 'mwanamke' | a - bha - kikulu 'wanawake' |

| | | |
|-----|--|---|
| | IT KNg Sh | IT KNg Sh |
| (b) | u - n - kangale 'mzee' IT KNg Sh | a - bha - kangale 'wazee' IT KNg - Sh |
| (c) | u - n - dimi 'mkulima' IT KNg Sh | a - bha - limi 'wakulima' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (vii) kwenye umoja zinawakilishwa na {n-} ya kiambishi ngeli //mu-// na kwenye wingi zinawakilishwa na kiambishi ngeli //bha-//.

Kwa ujumla, ni kwamba, nomino zilizooneshwa katika (i - vii) kiambishi //mu-// hujitokeza kama {mu-} ikiwa shina la nomino linaanza na konsonanti nazali /n/, hujitokeza kama {m-} ikiwa irabu /u/ itadondoshwa na shina la nomino linaanza na konsonanti za midomo. Pia, hujitokeza kama {mw-} kama shina la nomino linaanza na irabu (isipokuwa irabu /o/) ambayo haifanani na irabu ya KNg ambayo huyeyuka na kuwa kiyeyusho. Wakati mwingine, hujitokeza kama {n-} ikiwa irabu /u/ itadondoshwa na shina la nomino linaanza na konsonanti isiyo ya midomo. Pia, kiambishi //mu-// hujitokeza kama {mo-} ikiwa kinafuatiwa na irabu /o/ ambapo irabu /u/ ya kiambishi //mu-// hudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu /o/. Aidha, kiambishi //mu-// hujitokeza kama {ø-} ikiwa kiambishi //mu-// hakijitokezi kabisa. Kwa upande mwingine, utokeaji wa alomofu {mo-} katika ngeli ya 1 umoja unasababisha kutokea kwa alomofu katika wingi ambapo kiambishi //bha-// wingi hujitokeza kama {bho-} na kufanya kiambishi //bha-// kuwa na alomofu mbili ambazo ni {bha-} na {bho-}.

Ngeli ya 2, m-/mi-

Ngeli ya 2 katika lugha ya Kinyakyusa inawakilishwa na viambishi //m-// umoja na //mi-// wingi. Kiambishi msingi cha ngeli ya 2 umoja katika lugha ya Kinyakyusa ni //mu-//, lakini mabadiliko ya kurahisisha matamshi yametokea ambapo hamna/hazipo nomino zenye kiambishi //mu-// isipokuwa zenye //m-//. Hivyo, kiambishi //m-// umoja kina alomofu tatu ambazo ni {m-}, {mw-} na {n-}. Kiambishi cha wingi katika ngeli ya 2 ni //mi-// na kina alomofu mbili ambazo ni {mi-} na {my-}. Nomino za lugha ya Kinyakyusa zinazoingizwa katika ngeli hii ni kama zinavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

(i) m-/mi-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|---|--|
| (a) | i - m - piki 'mti' IT KNg Sh | i - mi - piki 'miti' IT KNg Sh |
| (b) | u - m - maghe 'kisu' IT KNg Sh | i - mi - maghe 'visu' IT KNg Sh |
| (c) | u - m - fwandilo 'jivu' IT KNg Sh | i - mi - fwandilo 'majivu' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (i) kwenye umoja zinawakilishwa na {m-} ya kiambishi ngeli //m-// na kwenye wingi zinawakilishwa na kiambishi ngeli //mi-//.

(ii) mw-/mi-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|--|--|
| (a) | u - mw - ifwa 'mwiba' IT KNg Sh | i - mi - ifwa 'miiba' IT KNg Sh |
| (b) | u - mw - ina kubwa 'shimo kubwa' IT KNg Sh | i - mi - ina makubwa 'mashimo makubwa' IT KNg Sh |
| (c) | u - mw - inuko 'mwinuko' IT KNg Sh | i - mi - inuko 'miinuko' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (ii) kwenye umoja zinawakilishwa na {mw-} ya kiambishi ngeli //m-// na kwenye wingi zinawakilishwa na kiambishi ngeli //mi-//.

(iii) n-/mi-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|--------------------------------------|---------------------------------------|
| (a) | u - n - tu 'kichwa' IT KNg Sh | i - mi - tu 'vichwa' IT KNg Sh |
| (b) | u - n - sana 'kiuno' IT KNg Sh | i - mi - sana 'viuno' IT KNg Sh |
| (c) | u - n - domo 'mdomo' | i - mi - lomo 'midomo' |

| | | | | | | | |
|--|----|-----|----|--|----|-----|----|
| | IT | KNg | Sh | | IT | KNg | Sh |
|--|----|-----|----|--|----|-----|----|

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (iii) kwenye umoja zinawakilishwa na {n-} ya kiambishi ngeli //m-// na kwenye wingi zinawakilishwa na kiambishi ngeli //mi-//.

(iv) mw-/my-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|--|---|
| (a) | u mw - elu 'mweupe' IT KNg Sh | i - my - elu 'weupe' IT KNg Sh |
| (b) | u - mw - enda 'nguo' IT KNg Sh | i - my - enda 'nguo' IT KNg Sh |
| (c) | u - mw - esi 'mwezi' IT KNg Sh | i - my - esi 'miezi' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (iv) kwenye umoja zinawakilishwa na {mw-} ya kiambishi ngeli //m-// na kwenye wingi zinawakilishwa na kiambishi ngeli //my-//. Kiambishi ngeli cha wingi kimewakilishwa na {my-} iliyotokea kutokana na mchakato wa uyeyushaji.

Katika nomino zilizooneshwa katika mifano ya (i - iv) kiambishi //m-// ambacho katika umbo la ndani ni //mu-// hujitokeza kama {m-} ikiwa kinafuatiwa na konsonanti zisizo za ufizi. Kiambishi //m-// hujitokeza kama {mw-} ikiwa shina la nomino linaanza na irabu isiyofanana na

irabu ya kiambishi //mu-/. Vilevile, kiambishi //mu-// hujitokeza kama {n-} ikiwa shina linaanza na konsonanti za ufizi.

Aidha, mifano ya nomino za wingi katika ngeli hii inaonesha kuwa kiambishi cha wingi ni //mi-// ambacho kina alomofu mbili. Kiambishi //mi-// hujitokeza kama {mi} ikiwa mchakato wa uyeyushaji katika nomino ya wingi haujatokea, na hujitokeza kama {my-} ikiwa mchakato huo umejitokeza katika nomino ya wingi **Ngeli ya 3, i-/ma-**

Ngeli ya 3 katika lugha ya Kinyakyusa inawakilishwa na viambishi //i-// umoja na //ma-// wingi. Viambishi vyote viwili havina alomofu kwa sababu michakato ya kifonolojia haijaathiri viambishi hivyo. Mifano ya nomino zinazolingia katika ngeli hii ni kama zinavyooneshwa hapa chini.

i-/ma-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|---|--|
| (a) | ∅ - i - kandi 'banzi' IT KNg Sh | a - ma - kandi 'mabanzi' IT KNg Sh |
| (b) | ∅ - i - ghondolo 'godoro' IT KNg Sh | a - ma - ghondolo 'magodoro' IT KNg Sh |
| (c) | ∅ - i - toki 'ndizi' IT KNg Sh | a - ma - toki 'ndizi' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika jedwali kwenye umoja zinawakilishwa na kiambishi ngeli //i-// na kwenye wingi zinawakilishwa na kiambishi ngeli //ma-//. Nomino za umoja katika ngeli hii zina muundo tofauti na

muundo wa nomino za umoja katika ngeli ya 1 na 2. Muundo wa nomino za umoja katika ngeli hii ni KNg + Sh kama ilivyooneshwa katika jedwali. Muundo ambao ni tofauti na ule wa ngeli ya 1 na 2 ambao ni IT + KNg + Sh.

Ngeli ya 4, ki-/fi-

Ngeli ya 4 katika lugha ya Kinyakyusa inawakilishwa na viambishi //ki-// umoja na //fi-// wingi. Kiambishi //ki-// umoja kina alomofu mbili ambazo ni {ki-} na {ky-}. Kiambishi //fi-// wingi pia kina alomofu mbili ambazo ni {fi-} na {fy-}. Nomino katika ngeli hii zinaoneshwa katika mifano ifuatayo:

(i) ki-/fi-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|---|---|
| (a) | i - ki - lundi 'mguu' IT KNg Sh | i - fi - lundi 'miguu' IT KNg Sh |
| (b) | i - ki - situ 'msitu' IT KNg Sh | i - fi - situ 'misitu' IT KNg Sh |
| (c) | i - ki - syanjo 'kichaka' IT KNg Sh | i - fi - syanjo 'vichaka' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (i) kwenye umoja zinawakilishwa na {ki-} ya kiambishi ngeli //ki-// na kwenye wingi zinawakilishwa na {fi-} ya kiambishi ngeli //fi-//.

(ii) ky-/fy-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|---------------------------------------|--|
| (a) | i - ky - inja 'mwaka' IT KNg Sh | i - fy - inja 'miaka' IT KNg Sh |
| (b) | i - ky - amba 'mlima' IT KNg Sh | i - fy - amba 'milima' IT KNg Sh |
| (c) | i - ky - ala 'ukucha' IT KNg Sh | i - fy - ala 'kucha' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Nomino zilizooneshwa katika (ii) kwenye umoja zinawakilishwa na {ky-} ya kiambishi ngeli //ki-// na kwenye wingi zinawakilishwa na {fy-} ya kiambishi ngeli //fi-//. Katika nomino zilizooneshwa katika (i - ii) kiambishi //ki-// hujitokeza kama {ki-} ikiwa shina la nomino linaanza na konsonanti, lakini hujitokeza kama {ky-} ikiwa shina la nomino linaanza na irabu. Kiambishi //fi-// wingi hujitokeza kama {fi-} ikiwa shina la nomino linaanza na konsonanti, lakini hujitokeza kama {fy-} ikiwa shina la nomino linaanza na irabu. Mabadiliko hayo husababishwa na mchakato wa kifonolojia wa ukakaishaji.

Ngeli ya 5, \emptyset -/ \emptyset -

Ngeli ya 5 katika lugha ya Kinyakyusa haina viambishi vinavyoiwakilisha katika umoja na wingi. Hivyo, ngeli hii huwakilishwa na // \emptyset -//. Nomino zifuatazo katika lugha ya Kinyakyusa huwekwa katika ngeli hii:

o-/o-

| Na. | Umoja | Wingi |
|-----|---|---|
| (a) | i - \emptyset - nywili 'nywele' IT KNg Sh | i - \emptyset - nywili 'nywele' IT KNg Sh |
| (b) | i - \emptyset - lefani 'kijiko' IT KNg Sh | i - \emptyset - lefani 'vijiko' IT KNg Sh |
| (c) | i - \emptyset - ngwata 'ndama' IT KNg Sh | i - \emptyset - ngwata 'ndama' IT KNg Sh |

Chanzo: Data za Uwandani (2017)

Senkoro (1997) na Ponera (2014) anaelezea dhana ya motifu kuwa ni msukumo au miegamo ambayo watunzi na wa kazi za fasihi hutumia kujengea miundo na maudhui ya kazi zao. Motifu huweza kuchukuliwa kuwa ni wazo la kazi ya kifasihi au kipengele cha kimuundo. Kulingana na Vogler (1998) na Nyamsenda (2015) motifu ni kipengele radidi cha kijadi au kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Mifano ya motifu za kifasihi anayoitoa ni pamoja na motifu ya safari; mama wa kambo, msako, mwanamke mshawishi, Bi kizee, mtoto wa ajabu, mtoto kigego, mnyonge anayemshinda mwenye nguvu, na motifu ya wema na uovu. Pia, Browning & Elmes (2015) wanaeleza kuwa motifu ni kujirudia kwa dhamira katika kazi za fasihi.

Kwa muhtasari tunaweza kusema kwamba motifu ni kipengele radidi cha kijadi kinachojirudiarudia katika fasihi ili kutimiza ujumbe fulani. Kwa mfano, kazi ya kisanaa huweza kuwa na motifu ya ushujaa, msako, safari, kifo, ushindi, ushawishi, wema, kukataliwa, uovu, uchawi, uganga na tiba na kusamehewa. Hivyo, katika makala hii, motifu imetumika kama njia au mbinu ya kukuza ama kuisisitiza jambo ambalo limejitokeza mara nyingi katika tamthiliya teule.

Mada Iliyochunguzwa

Ingawa tamthiliya ya Kiswahili huangazia masuala mengi yanayoithiri jamii, uchunguzi kuhusiana na tamthiliya umekuwa ukijikita zaidi katika uhakiki wa vipengele vya maudhui na fani yake. Ili kupanua mawanda ya kuihakiki tamthiliya, kuna haja ya kutilia mkazo uhusiano uliopo kati ya tamthiliya na mbinu nyingine za kisanaa, zikiwamo za kimotifu. Kwa kufanya hivyo, utanzu huu utakua na kukomaa kupitia uhakiki wake katika mikabala ya fani mbalimbali. Uchunguzi huu ulizingatia nafasi ya tamthiliya teule katika uchunguzi wa utokeaji wa motifu na umuhinu wake. Mkazo ulizingatia kwamba, kwa muda mrefu, tamthiliya ya Kiswahili ni mojawapo ya vyombo imara vinavyohakiki na kusawiri hali halisi inayotoa picha ya motifu mbalimbali kwa kuonesha masuala nyeti yanayoihusu jamii. Hali hii huifanya tamthiliya kuwa chombo muhimu kinachoelewa jamii kwa undani.

Lengo na Upeo wa Utafiti

Lengo la uchunguzi huu lilizingatia nafasi ya tamthiliya teule katika utokeaji wa motifu na umuhinu wake. Uchunguzi ulikusudia kubainisha aina za motifu katika tamthiliya zilizolengwa. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani uliohusisha uhakiki tamthiliya teule. Uchunguzi ulitekelezwa katika maktaba za Chuo Kikuu cha RUCU, MUCE na Chuo Kikuu cha Iringa. Watafiti walidurusu kazi tofauti mbalimbali zilizohusiana na mada iliyolengwa, pamoja na misingi ya nadharia ya Usosholojia. Utafiti huu ulihakiki wa nafasi ya tamthiliya teule katika utokeaji wa motifu na umuhinu wake. Utafiti ulijikita katika vitabu vya *Sundiata* (2011) na *Fumo Liongo* (2009).

Nafasi ya Nadharia katika Uchunguzi na Uhakiki wa Kifasihi

Nadharia ya Usosholojia iliasisiwa na Hippolyte Taine; na ilianza kujitokeza karne ya 19 na kushamiri karne ya 20 barani Ulaya (Njogu &

Chimerah, 1999). Mojawapo ya misingi yake ni kuyatazama mazingira ya asili ya jamii kuwa ndio huamua namna kazi ya kifasihi inavyotakiwa kuwa. Aidha, huitazama kazi za kifasihi kuwa ni nakala ya tabia; na ni kiwakilishi halisi cha jamii fulani (Shorter, 1969 & Selden, 1990). Pia, hutumika kuikabili fasihi kwa namna inavyohusiana na mazingira ya jamii.

Kwa upande mwingine, fasihi hutazamwa kama kitengo pekee kilicho na uwezo wa kuakisi sayansi na utamaduni wa jamii; na ni usawiri mkamilifu ambao huyasawiri maisha kwa undani na huyachunguza kwa mtazamo mpana (Narizvi, 1982). Mtafiti alijihusisha na uchunguzi wa nguvu za kijamii zinavyohusiana na nguvu za kisanaa. Uchambuzi ulizingatia kwamba, kwa kawaida, kazi ya fasihi hudhibitiwa na miundo iliyopo katika jamii kwa kuzingatia uhusiano wa wanajamii katika mienendo yao ya kila siku (Cosser, 1963). Motifu zilizobainishwa katika vitabu teule zilitazamwa kama zao na kiungo maalum cha mahusiano ya jamii iliyochunguzwa kwa kuzingatia historia yao, falsafa yao, mila na desturi zao, uchumi wao na siasa zao.

Kwa ujumla, nadharia hii huitambua nafasi kubwa na muhimu inayochukuliwa na muktadha wa kijamii katika uhakiki wa motifu za kijadi kwa kuzingatia umithilishaji wa hali fulani za ulimwenguni (Msokile, 1993). Kwa msingi huo, motifu zilizochunguzwa zilitazamwa na kufasiriwa ndani ya muktadha wa jamii ya mwandishi na historia yake. Mtafiti alichunguza uhusiano uliopo baina ya wahusika na mienendo ya shughuli zao za kila siku, falsafa zao na mitazamo yao. Pia, alichunguza uhusiano wao, historia na maendeleo ya jamii yao katika nyanja zote za kijamii. Hali hii ilimwezesha mtafiti kuzichunguza motifu katika vitabu teule kwa kina ili kubaini mambo yaliyolengwa kulingana na utamaduni, historia, mila na desturi zao. Kwa hiyo, nadharia ya Usosholojia ilikuwa muafaka katika uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data zilizolengwa katika makala haya.

Dhima na Utokeaji wa Motifu katika Tamthiliya Teule za Emmanuel Mbogo

Katika makala hii tumebaini kuwapo kwa motifu mbalimbali zenye dhima tofauti tofauti katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo za *Sundiata* na *Liongo*. Utokeaji wa motifu kama kipengele radidi cha kimuundo umeshikamana kikamilifu na maudhui yaliyojengwa katika jamii iliyolengwa kwa kuzingatia wakati na muktadha wa uandishi wa mwandishi. Motifu zilizomo zimetumika kama kiungo maalumu cha kimuundo na kimaudhuikatika kufanikisha kusudio la kifasihi. Baadhi ya motifu zilizochunguzwa katika makala hii ni pamoja na ile ya unguli, motifu ya sihiri, matifu ya msako na motifu ya safari. Motifu hizo zimefafanuliwa kama ifuatavyo:

Motifu ya Unguli

Nguli au shujaa ni mtu jasiri mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo hata kama ni ya hatari (TUKI, 2004). Hivyo, ushujaa ni ujasiri ambao mtu huwa nao katika kulikabili jambo bila hofu au kwa uhodari. Uchunguzi wetu umegundua kuwa motifu hii inatokana na mambo ya kishujaa ambayo nguli ameweza kuyafanya ili kudhihirisha ujasirii wake. Katika tamthiliya ya *Sundiata*, mwandishi ameonesha namna Sundiata alivyopambana kikamilifu dhidi ya uongozi dharimu wa Sumanguru. Sundiata alipigania haki na demokrasia ya kweli katika jamii yake kama mwandishi anavyoeleza:

Vita hivi havitakuwa na mwisho hadi wafalme wote wa Mali watupe silaha chini, wasalimu amri na kukiri kuwa Mali ni moja chini ya Mansa Sundiata. Tunahitaji kukomesha udhalimu, ufisadi na ufisidi. Tunahitaji kuondoa hofu na utawala wa mabavu miongoni mwa raia wetu,

tunahitaji kuleta maendeleo na ustawi miongoni mwa watu wetu... (Mbogo, 2011: 57).

Katika nukuu hii inaonesha unguli katika kupigana vita ili kukomesha udhalimu, ufisadi na ufisidi uliokuwa umetamalaki katika jamii yao. Sundiata alijitoa mhanga ili kuhakikisha maendeleo na ustawi kwa wanajamii unajengwa na kuimarishwa kwa manufaa ya jamii nzima. Aidha, kupinga suala la kuwajaza hofu na vitisho wanajamii ambako kunaweza kuzuia shughuli za kimaendeleo. Sundiata anaihamasiha vita na kujitoa muhanga ili kuifia nchi kwa manufaa ya jamii nzima kama inavyooneshwa pale Sundiata anaposema:

...Hakuna kurudi nyuma sharti tuwe tayari kuifia nchi na watu wetu. Vita hivi vikiisha na amani kuturudia: Wamandingo wanahitaji maendeleo. Kilimo, uvuvi na ufugaji sharti kiimarishwe...(Mbogo, 2011: 58).

Katika motifu hii, inaonesha ujasiri kwa kupambana na adui kwa kujitoa muhanga kupigania nchi na kurejesha amani na maendeleo kwa wananchi wote. Mwandishi katika kazi teule anajaribu kutuonesha kuwa ili jamii ipate maendeleo lazima kuwepo na wazalendo wanaoipigania nchi kwa hali na mali, hata kuifia, ilimradi tu maendeleo yanapatikana.

Pia, katika tamthiliya ya *Liongo*, motifu hii imejitokeza kutokana na uwezo wa Liongo kukabiliana na maadui zake, kupigania haki na demokrasia ya kweli na maendeleo ya jamii yake. Katika tamthiliya hii, motifu ya unguli hujidhihirisha kwanza, kwa kitendo cha Liongo kupigania haki, kupinga utawala dharimu wa Mringwari, ushujaa wa kutoroka gerezani, kupambana na kuwaua askari wawili miongoni mwa watatu waliotumwa na mfalme wamuue. Pia, alipambana na kupigana na adui Sango Vere na kumshinda. Unguli huo hudhihirika kwa kupambana bila hofu kama inavyojidhihirisha kwa kusema:

...Macho yako yaliwakabili askari wako ukatutangazia: ufalme wa Pate umo katika hatari ya kuanguka. Wabuu wa Sango Vere ... wamekwishaingia Kaskazini na kuiteka ardhi ya Wabajuni!... Kufumba na kufumbua simba...wakawa wamezifunga njuga kukicheza kitali na mabuu. Adui tumemshinda,na mateka tumechukua... (Mbogo, 2009: 9).

Nukuu hii imeonesha wazi hali ya umoja katika mapambano ya kumkabili adui kwani umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Hivyo, jukumu la kuwa shujaa na ushindi linahitaji dhana ya umoja na mshikamano. Liongo alikuwa jasiri kwa kukemea udhalimu uliokuwa unafanywa na mfalme Mringwari kwa kuwaua watu wanaopenda haki itendeke. Matokeo ya harakati za Liongo zilizaa matunda mabaya ya kidhalimu zaidi, hasa pale mfalme Mringwari anapoamuru kumkamata Liongo, kumtesa na kumfunga jera; na baadaye kufanya jaribio la kumuua kupitia askari wake. Kwa ujumla, hali ya kupigania haki na demokrasia katika jamii linahitaji kujitoa mhanga, umoja na ushirikiano na kujenga uzalendo wa dhati baina ya wapambanaji.

Motifu ya Safari

Vogler (1998) anaeleza kuhusu motifu za safari za shujaa kuwa kwa kawaida huanzia pale shujaa anapoanza kukua binafsi ili kutafuta kushinda mashindano, kuondoa machungu na kutafuta mapenzi na haki. Katika safari hii, Sundiata anatafuta kupata haki yake ya urithi wa ufalme na kuitawala Mali ambayo imechukuliwa kimabavu na Dankarani. Suandiata alianza kujipambanua kama shujaa, hasa aliporejea kutoka msituni na kuingia ikulu ili kupigania kiti cha ufalme. Mwandishi anaeleza kama alivyomnukuu Dankarani akisema:

*Taarifa ni kuwa, Sundiata amerejea toka msituni.
Alifika kwangu alfajiri kutaka aongee name,
lakini moyo wangu ulisita kumpokea...amekuja*

ikulu leo alfajiri, mishipa imemsimama. Akadai eti mimi Dankarani ning'atuke, nimwachie yeye Sundiata kiti hiki cha Ufalme; nilivue eti alivae yeye taji hili la ufalme na mamlaka. Bwana Sundiata alitaka kuingia kwa nguvu (Mbogo: 2011: 16-18).

Katika motifu hii, Sundiata anaanza kushughulikia suala la ukombozi na kutaka haki katika mambo mbalimbali. Kwanza anataka manju wake aliyepotea katika mazingira tatanishi arudishwe mara; na kama hammpati, basi kwa sime damu ya mahasimu hao itamwagika li iwe sadaka kwa miungu na mizungu ya wamandingo. Aidha, Sundiata anakejeli uongozi wa dhalimu wa Dankarani kwa kueleza kuwa wangejua utamaduni na mapisi ya nchi, wasingemvalisha taji sokwe mtu ili kuitawala Mali, nataka kukueleza wewe na balaza lako linaloongozwa na mwanamke kuwa nitaitafuta taa ya ukombozi mpaka niipate. Motifu hii ya safari imeonesha umuhimu wa usawa na haki za binadamu ili kutokomeza tamaa ya madaraka, hila na udhalimu dhidi ya raia wasio na hatia.

Aidha, safari ya Sundiata kwenda Mema ilisababishwa na mfalme Dankarani kutwaa Taji la Ufalme kwa mabavu na kwa mlungula; kisha kumwamuru na kumfukuza Sundiata mrithi wa huo ufalme kwamba atoke katika nchi yake. Hata hivyo, Sundiata alilazimika kwenda ugenini katika mji wa Mema unaoongozwa na mfalme Tunkara, huko anapokelewa na kujiunga na jeshi la nchi hiyo na kujifunza mambo mengi ya kijeshi.

Akifafanua hatua mbalimbali za motifu ya kisafari, Senkoro (1997) anaeleza kuwa safari ya kwanza ya nguli ni ile ya kawaida inayohusu ukuaji wa mhusika kimwili na akili, lakini safari ya pili, huiita safari ya ndani ambayo huambatana na busara, hekima, uamuzi na utambuzi wa

mhusika na yale anayokumbana nayo. Mhusika huwa na kiwango cha ujuzi cha safari kwa kuwa hapo ndipo mhusika hufikia kiwango cha kupata maarifa na uzoefu mpya baada ya kupitia vikwazo vingi, mateso na hata kwenda uhamishoni. Hivyo, maarifa hayo huambatana na hulka ya unyenyekevu, werevu, wepesi wa kufanya maamuzi na suala la uwazi. Hapa tunaoneshwa Sundiata akihutubia majeshi yake huko ugenini Mema akiwa tayari kupambana katika kumkabili adui dhidi ya udhalimu, uovu, hujuma, ukosefu wa haki na demokrasia. Sundiata alisema:

Tupo askari wa kutosha. Jeshi la Mema limo mikononi mwangu. Jeshi la Wagadu lipo chini yangu. Jeshi la Fran Kamara pia liko nyuma yangu. Vita hii haitakuwa na mwisho hadi wafalme wote wa Mali watupe silaha chini na kukiri kuwa, Mali ni moja chini ya Mansa Sundiata. Tunahitaji kuondoa hofu na ufisadi na ufisidi. Tunahitaji kuondoa hofu na utawala wa mabavu miongoni mwa raia wetu. Tunahitaji kuleta maendeleo na ustawi miongoni mwa watu wetu (Mbogo, 2011: 57).

Sundiata katika nukuu hizo anatangaza kutoisha kwa vita mpaka tabaka kandamizi litakapoachana na ukandamizaji kwa raia. Hata hivyo, kupitia nukuu hii utafiti umegundua kuwa safari ya Sundiata ilikuwa na nia ya kutaka kukomesha uongozi wa mabavu, rushwa na kuleta maendeleo na ustawi miongoni mwa raia. Karl Marx anaamini kuwa nyenzo za uzalishaji mali kama ardhi, mitaji, ujasiriamali na nguvu kazi zikiwa zinamilikiwa na mtu mmoja mmoja, kamwe haziwezi kuitoa jamii katika mfumo wa unyonyaji. Hali hii huifanya jamii kuwa na watu wengi ambao ni maskini sana na watu wachache kuwa matajiri sana (Marx & Engels, 1848). Nyenzo za uzalishaji mali zinapomilikiwa na watu wote kupitia serikali yao, upo uwezekano mkubwa wa kupunguza na kuondoa kabisa matabaka ya walionacho na wasionacho katika jamii. Kwa ujumla,

nguli anaweza kuondoka eneo moja na kwenda eneo jingine ili kutafuta uhuru binafsi ama kutafuta suruhu ya changamoto za jamii yake (Mwangoka, 2011).

Motifu ya Msako

Motifu ya msako katika makala hii inaonesha kupitia Sundiata ambaye alipoishi uhamishoni huko Mema kwa mfalme Tunkara, aliweza kujifunza mengi kuhusu masuala ya ulinzi wa kijeshi na maendeleo mengine kwa manufaa ya jamii na umma kwa ujumla. Haja ya kurudi katika jamii yake kusaka cheo na madaraka aliyoporwa inamjia na kuanza kufanya utaratibu sahihi wa namna ya kurudi kuikomboa jamii yake. Hivyo, anaona ni vema sasa arudi aikomboa jamii yake ya Wamandigo kwani ilikuwa imevamiwa na adui Sumanguru. Sundiata aliamua kumuaga Tunkara akisema:

Baba mfalme siku zangu za kuishi nawe na kukutumikia sasa zimekwisha. Utanisamehe baba, lakini wakati wangu wa kuliongoza jeshi ili kuwakomboa Wamandigo sasa umewadia. Shukurani zangu zisizo kifani kwa wema na fadhili nyingi ulizotutendea. Mimi binafsi nimejifunza mengi hususani kunikuza na kunikomaza kijeshi. Lazima nitimize kazi inayonikabili mbele yangu (Mbogo, 2011: 37).

Makala hii imegundua kuwa motifu ya msako ya Sundiata kutaka kurudi Mali umeonesha dhana ya viongozi kutojali mafanikio ya raia kwani anapotaka kurudi kuikomboa Mali anazuiliwa ili tu amnufaishe mfalme Tunkara kwa kupambana na maadui wa nchi yake. Jambo hili linaonesha msimamo wa Sundiata kutaka kuikomboa Mali mikononi mwa Sumanguru kutokana na udhalimu anaoifanyia jamii yake. Sundiata haoni sababu ya kuendelea kukaa uhamishoni wakati jamii yake iko hatarini. Kwa kawaida, shujaa anaweza kurejea kutoka uhamishoni ili

kuikomboa jamii yake Volger (1998). Hii hudhihirisha motifu ya msako ya shujaa kurudi katika nchi yake ili kufanya ukombozi.

Katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*, motifu ya safari na msako, kwanza inaanza kwa mbinu ya mrisho nyuma, kwani shujaa Fumo Liongo anaeleza namna walivyoenda kupigana baada ya kurudi kutoka vitani wakiwa na ushindi. Liongo anamkumbusha mfalme jinsi walivyopambana usiku ule wa giza, rewa ya ikulu ilipolia kualika kitali. Wanaume... tulizinduka na bila ya kuwaaga tuwapendao tulizinyakua silaha zetu tukaja mbio ikulu kwa lufufu. Ukatatangazia kuwa ufalme wa pate upo katika hatari kuanguka. Wabuu wa Sango Vere wamekwishaingia Kaskazini na kuiteka ardhi ya Wabajuni. Kufumba na kufumbua simba, chuwi na nyuki wa Pate wakawa wamezifunga njuga kukicheza kitali na mabuu. Adui tulimshinda na mateka ya ngawira tumechukua....(Mbogo, 2009: 9).

Maelezo yanadhihirisha kuwa nguli na jeshi lake waliweza kupambana na adui na kumshinda kutokana na uhodari wa jeshi lake. Aidha, ni motifu ya msako ya Liongo kwenda Ikulu inatokana na mwaliko aliopewa na mfalme Mringwari. Sababu ya safari hii pia ni kupeleka zawadi ya Mringwari toka kwa mfalme wa Gala iliyoletwa na Zahidi mwanae kwa sababu raia wake aliruhusiwa kuzaa na Liongo kama heshima ya urijali wake.

Motifu ya Sihiri

Sihiri ni kitendo cha kufanya uchawi, kuroga (TUKI, 2004). Kulingana na Mutiso (2012) hirizi kama kisawe cha sibirini kitu kinachomkinga mwanadamu kutokana na matatizo. Pia ni kitu kinachoweza kumkinga mhusika dhidi ya uovu au maovu kama kumkinga na shambulio la wezi, uchawi, husuda, mikosi. Aidha, humsaidia mhusika kutekeleza maazimio yake kama vita, ndoa, kazi n.k. Hivyo, tunawza kusema kuwa sihiri ni falsafa yenye dhana ya kitu chenye kuaaminiwa kuwa ni dawa, kitu

chenye nguvu kinachoweza kumkinga mtu na madhara, azima, talasimu, dawa, kago, pagao, amali, au kuleta heri na kutibu. Katika tamthiliya za Kiswahili, motifu hii imeweza kujitokeza katika mazingira mbalimbali kwa kusudi maalumu.

Kwanza, ni sihili iliyohusu kutegua uwete wa Sundiata. Hapa sihiri ilitumika kama dawa ya kutibu uwete wa Sundiata kupitia dada yake Kolonkani. Kolonkani ansema:

Chini ya mbuyu, juu ya madhabahu, tulichinja mnyama, tukatoa sadaka ya damu ya kondoo mweusi. Wahenga wakalipokea tambiko; wakanywa makombe ya damu ya sadaka. Katikati ya ibada, shangwe na masujudio haya, tulifunuliwa siri na kutuonesha opoo la kutegua sihiri ya uwete wa kakangu Sundiata. [Akitoa kibuyu chenye dawa. Sundiata anakunywa. Anamvalisha kidani chenye hirizi. Anatoa majani na kumpiga nayo Sundiata kichwani] Balla, ima faima, leo simba, mfalme wa Mali, mwana wa Sogoloni atakanyaga ardhi kwa miundi yake miwili. Anamchanja chale Sundiata mwili mzima kisha anampaka mavumba. Dawa inawasha hiyo, Sundiata anafurukuta pale chini ... wanaume wamebeba gogo zito na kulitua mbele ya Sundiata.

Sundiata anasota hadi kwenye pande la chuma. Analikagua, anatemea mate katika viganja na kujaribu kulisimamisha... WAPI! Mara ya tatu: linasimama. Sasa analishika sawa sawa... anafumba macho... na kwa mpigo mmoja JUU-! Anainuka na kusimama Sundiata hajasimama

upande ule nalo wima. (Mara tena anarudi akiwa upande na upondo, anaonesha majigambo kisha anaungana na wacheza ngoma) (Mbogo, 2011: 8 - 9).

Kupitia nukuu hii, makala hii imegundua kuwa kiutamaduni kuna falsafa ambazo zinawatesa watu waonekane dhaifu kwa sababu ya uchu wa madaraka kwa kutumia hila za kisihiri. Tamthiliya ya *Sundiata* imeonesha kuteguliwa kwa tigo la uwete alilotegeva *Sundiata*. Tigo hilo limeweza kuteguliwa kwa kafara ya sadaka ya damu ya kondoo mweusi. Hivyo, kupitia nadharia ya usosholojia sihiri imetumika kama uganga na tiba kwa kumvisha *Sundiata* kidani chenye hirizi na kunyweshwa dawa ambayo ndiyo vilichangia kupona kwake. Pia, sihiri kama falsafa yenye dhana ya kitu chenye kuaminiwa kuwa ni dawa, kitu chenye nguvu na kinachoweza kumkinga mtu na madhara (Mulokozi, 2002). BAKIZA (2008) wanaunga mkono hoja hii kwa kusema kuwa, Waswahili wana falsafa ya kupunga pepo kuwa ndiyo dawa ya wagonjwa wao badala ya kuwapeleka hospitali. Hivyo motifu hii inajaribu kuonesha uovu wanaofanyiwa watu kwa hila kutokana na roho ya wivu na chuki, hasa kutokana na sababu za ubinafsi, tamaa na uchu wa mali na madaraka.

Kupitia tamthiliya hii, makala hii imegundua kuwa kutamani madaraka kunawafanya watu watumie uganga au sihiri kuwapoteza watu wanaoonekana kuwa na nyota ya kupata nafasi za uongozi kama Sassuma alivyohofia kuwa *Sundiata* anaweza kupata kiti cha ufalme. Matokeo yake anajaribu kufanya mitego ya kiulozi ya kumuua *Sundiata* ili mwanae Dankarani achukue kiti cha ufalme. Hii inatokana na tamaa ya Dankarani na mama yake Sassuma kuyataka madaraka ambayo kiutamaduni alitakiwa apate *Sundiata*. BAKIZA (khj) wanatoa angalizo kuwa wapo watu wengine huwa na tabia ya kuwaonea kijicho wenzao katika vitu waliyonavyo kisha huviharibu visiendelee kwa imani za kishirikina. Jambo hili hujidhihirisha pale Sassuma anapoandaa mipango

ya kufanya sihiri ili kumkatili Sundiata asipate ufalme, hivyo, kupitia kazi teule, makala hii imegundua kuwa motifu ya sihiri imetumika katika kuangamiza roho za watu kwasababu ya uchu wa madaraka. Kwa upande mwingine, sihiri huweza kutumika kuwa ni mbinu ya kutimiza ukatili kwa kuharibu akili za watu na kuwafanya vizuu ili kupata utajiri (Mbogo, 2008). Kwa kutekeleza uharibifu huo, sihiri na hirizi iliweza kutumika kudhihirisha uovu miongoni mwa jamii kwa kutumia ushirikina kama Sassuma alivyolivyo fanya kuitafuta na kuiondoa roho ya Sundiata kwa njia ya ulozi.

Aidha, Sumanguru ni kiongozi ambaye ni katili na ukatili wake unatiwa nguvu na sihiri alizokuwa nazo. Hivyo, ili kuuondoa ukatili wake kwa raia ilihitajika kuwa na nguvu za sihiri pia. Masuala ya uchawi, ushirikina, uganga na tiba ni vyombo vya kijadi vinavyojishughulisha na masuala ya tiba na kinga katika jamii (Shimweta, 2015 & Mwangosi, 2018). Hapa, Koroma anang'atuka kutoka jeshi la Mringwari na kujiunga na jeshi la Sundiata ili kupambana na udhalimu wa Mringwari na anaeleza namna ya kujikinga na uchawi wa Sumanguru na namna ya kuutegua uchawi wake. Hivyo, Koroma na Nana wanatoa siri za nguvu za sihiri za Sumanguru. Koroma anaeleza:

*Sumanguru ni mtawala katili anayeabudu
ushirikina, anayefuga majini yanayomsaidia
kuitawala Soso. Kila usiku, usiku wa manane,
Sumanguru na magwiji wake hutoa sadaka ya
damu ya fahari. Tena magwiji wake
wametendesa katika falaki ya ulozi wa jua,
mwezi, nyota na sayari nyingine. Naye, Nana
anaeleza kwamba Sumanguru alinifunulia siri.
Alisema: mimi siuliwi kirahisi. Mtu akitaka
kumuua Sumanguru, kwanza atafute jogoo
mweupe pee! Amchinje na damu yake anyunyize
mara tatu kuizunguka ngome yangu. Kisha*

ang'oe karanga gumba achambue na kuyasambaza majani yake kuzunguka ngome ya Soso. Akifanya haya yote ataivunja ngome na kuniua mimi Sumanguru (Mbogo, 2011: 58 - 68).

Nukuu hii inaonesha namna viongozi wanavyotumia nguvu za sihiri, na mabavu katika kuongoza jamii zao. Wakati mwingine, hulindwa na kuamini nguvu za sihiri jambo linalosababisha kuwatia watu hofu, mashaka na kukwama kwa maendeleo ya wanajamii. Hivyo mwandishi anaonesha kuwa wakati mwingine ili kuondoa hofu, udhalimu, ufiisadi na utawala wa mabavu kama wa Sumanguru lazima sihiri ihusike, kwani mabavu hayo yana mizizi ya sihiri. Binadamu huweza kusaidiwa na nguvu nyingine zilizo nje ya uwezo wa kibinadamu pale uwezo wa kibinadamu unapozidiwa (Mgogo, 2017). Hapa ndipo tunamuona Sundiata anakubaliana na ushauri aliopewa, anaamua kutoa kafara kwa miungu ili imsaidie kupambana na Sumanguru.

Katika tamthiliya ya *Liongo*, motifu ya sihiri inayojitokeza ni ile iliyomuhusu Liongo kuonesha kuwa uwezo wa nguvu zake na maarifa ya kukabiliana na maadui ulitokana na uwezo wa sihiri iliyoambatana na kitovu chake. Mutiso (2012), Mohamed (2002) & Mbiti (2011) wanaeleza kuwa hirizi ni kitu kinachoweza kumkinga mhusika dhidi ya uovu au maovu, kama kumkinga na shambulio la wezi, husuda, mikosi. Aidha kumsaidia mhusika kutekeleza maazimio yake kama vita, kazi n.k. katika kujua nguvu ya sihiri ya Liongo iliyokuwa ikimkinga na kifo, uovu, vita n.k., hapa Zahidi anafanikiwa kuidodosa siri ya sihiri hiyo kama ifuatavyo:

Nilimuuliza, Baba mpenzi ni kitu gani kiwezacho kukuua? Akasema "Zahidi mwanangu, mimi ni Fumo Liongo. Mimi ni Simba wa Pate. Hakuna mwingine yeyete ajuaye siri ya uhai na ufu wangu ila mimi na yeye Muumba wangu"

“Mwanangu Zahidi. Mimi mkuki hauniui, shoka haliniui, mimi mshale hauniui, mimi kisu hakiniui. Kitu chochote mimi hakiniui. Ila ukitaka kuniua mimi fanya bidii utafute sindano ya shaba. Uchukuwe sindano ya shaba; kwa sindano ya shaba unichome nayo kitovuni. Ukinichoma nayo kitovuni basi mie Fumo Liongo nitakufa (Mbogo, 2009: 38).

Kwa nukuu hizi sihiri iliyokuwa siri inakuwa wazi kupitia Zahidi mwana wa Liongo ambaye analubuniwa kwa ahadi ya zawadi ya mke, kazi na mali toka kwa mfalme Mringwari ili kumwanganamiza Liongo. Tamaa ya mali na rushwa imekuwa ni chanzo kikubwa cha kuzuia ujenzi wa jamii mpya katika bara la Afrika na kusababisha kudolola kwa maendeleo (Mbogo, 1997).

Motifu ya Kifungo

Kifungo ni adhabu ya kumweka mtu jela. Katika tamthiliya teule wahusika mbalimbali wameonekana kukumbwa na adhabu ya kuwekwa jela kwa sababu ya kutetea haki. Katika tamthiliya ya *Liongo* tunaona kifungo kinachotokea ni kutokana na dhana ya watawala wa bara la Afrika kutopenda kukosolewa (Mbogo, 2015). Liongo anapomkosoa Mfalme Mringwari ndipo anapoamuru akamtwe awekwe ndani na kuteswa. Hii inaoneshwa pindi Liongo akiwa ikulu kwa Mringwari, kama Liongo anavyoeleza:

Mringwari Mtukufu Mfalme. Mimi siamini kuwa mzee Msheki ana maradhi yoyote yaliyomlaza kitandani. Bali maradhi hayo yamemlaza chini ardhini. Msheki kauawa na Mazabania wako wa hapa ikulu. Semeni kama nisemavyo ni uzushi, Mtukufu Mfalme wa Pate? Baada ya maneno hayo, mfalme alitoa amri, mwekeni mahabusu na

chini ya ulinzi mkali. Kila asubuhi na jioni mrambeni mwilini kwa mijeledi ya mkia wa taa mpaka tutakapojua hatima yake (Mbogo, 2009: 22).

Kwa hiyo, kupitia motifu ya kifungo cha Liongo inaonesha wazi kuwa utawala wa Mringwari ulikithiri mabavu, uovu na kuwanyima watu haki ya kutoa maoni, kubadilishana mawazo ya msingi yenye lengo la kuchochea usawa wa binadamu na maendeleo yake. Mfalme hakupenda kuambiwa ukweli na kukosolewa, vinginevyo mkosoaji anajikuta mikononi mwa nguvu ya dola. Hii ndiyo tabia ya baadhi ya viongozi wengi wa vyama na serikali katika jamii nyingi za Kiafrika. Pamoja na mateso yote aliyokuwa akiyapata Liongo akiwa jela tunaona anafanikiwa kutoroka anarudi nyumbani ili kusaka usalama wake japo, hata huko anaona usalama wake utakuwa hatarini, hivyo anaamua kwenda msituni ili kuepuka mateso ya Mringwari.

Motifu ya Kifo

Mwandishi wa tamthiliya ya Sundiata ameonesha anguko linayomkuta mhusika Sundiata kuwa ni kutokana na hulka ya kufurahia ushindi na kufanya uzembe kwa kusahau kuweka ulinzi wa kutosha katika kulinda shughuli nzima ya kusherekea ushindi wake. Hivyo kupitia hila za Sassuma mpinzani wake Sundiata, ndipo Sundiata anakumbwa na kifo. Kama inavyoonekana:

Sassuma alivyovalia, hatambuliki. Anamsogelea Sundiata; anainua taji juu ili amvike. Sundiata anasita, lakini akina mama wawili wanamhimiza asogee, ainame. Sundiata anasogea, anainama. Sassuma anamvika taji kwa mkono wa kushoto na kumchoma kisu mara tatu kwa mkono wa kulia. Wanawake wote wanakimbia kwa mshituko

*na mshangao. Sundiata anayumba kwa uchungu
(anaanguka anakufa) (Mbogo, 2011: 18 - 37).*

Hata hivyo, Aristotle (1958) anatueleza kwamba mhusika hapewi nafasi ya kufurahia ushindi wake kwani anapomaliza mapambano na kupata ushindi mhusika huyo lazima akumbwe na tanzia. Hata hivyo tunaona kuwa nguli Sundiata anapata tanzia kutokana na kusakamwa na mazingira yanayomzidi uwezo ambayo yamegubikwa na uroho wa madaraka na ubinafsi wa Sassuma kupigania kiti cha ufalme kikaliwe na mwanae.

Katika tamthiliya ya *Liongo* inatuonesha Liongo anauawa kupitia mwanae chanzo kikiwa ni uchu wa madaraka wa Mringwari na usaliti na tamaa ya zawadi alizoahidiwa Zaidi na Mfalme Mringwari kuwa akifanikiwa kujua siri ya kifo cha Liongo na kutekeleza mauaji, atapewa zawadi ya mke, madaraka, na mali. Hivyo Zahidi anafanikiwa kuumua Liongo kwa kumchoma na sindano ya shaba kitovuni na kukimbia. Kama inavyojidhihirisha:

Liongo anasikika akikoroma. Zahidi anainuka taratibu, anamtazama Liongo. Anamwita Liongo!) Baba... (kimya. Anatoa sindano... jogoo anawika tena...kisha tena sauti za mbweha na fisi. Zahidi anamnyemelea na kumchoma Liongo sindano ya kitovu na kukimbia...sauti za radi...kunapita muda mfupi... kisha Liongo anainuka, anashika tumbo kwa maumivu... anaichomoa ile sindano na kuikodolea macho... Zahidi mwanangu umeniua... (Mbogo, 2009: 42-46).

Katika tamthiliya hii *Liongo* kama shujaa anakufa kwasababu ya kutoa siri ya nguvu zake kwa Zahidi mwanae, siri ambayo anatueleza kuwa

aliijua yeye tu na Muumba wake hata mama yake hakuijua. Kwa mujibu wa Aristotle (khj) na Semzaba (1997) wanaeleza kuwa tanzia ya nguli huwa inasababishwa kutokana na nguli kuandamwa na jamii yake, uzembe au kuzidiwa nguvu na adui. Lakini Volger (khj) katueleza kuwa motifu ya kifo huweza kumpata nguli pale anapokuwa na woga kutokana na upinzani anaoupata. Utafiti umegundua kuwa katika tamthiliya ya Liongo msanii hatuambii kwamba labda nguli Liongo anatoa siri kuhusu nini kinaweza kumuua kwamba, ni kwa sababu ya woga, bali ni kutokana na kusakamwa na mazingira yanayomzidi uwezo ambayo yamegubikwa na uroho wa madaraka wa Mfalme Mringwari ambayo yanakamilishwa na usaliti wa mwanae Zahidi. Hata hivyo utafiti wetu ulibaini kuwa licha ya kuwepo mabadiliko katika maisha na fikra za binadamu bado huweza kukumbwa na usaliti kwasababu ya kurubuniwa na kusababisha mauti kwa wengine, hata hivyo bado janga limpatalo mhusika katika tanzia halimhusu yeye tu binafsi bali linavuruga hali nzima ya utulivu ya jamii yake. Campbell (1968) ushindi anoupata nguli ni wa jamii nzima na si wake binafsi, pia watu waumie pamoja naye pale inapotokea ameumizwa. Hapa tunaona pindi Liongo anapopata mauti jamii inasikitishwa na kupatwa na hofu.

Hitimisho na Mapendekezo

Makala hii imetazama utokeaji wa motifu katika kazi teule kama kipengele kinachosisitiza maudhui/dhamira. Makala yametupa mwanga wa kusawiri dhamira msisitizo kupitia ule utokeaji wa motifu. Aidha, kupitia utokeaji wa motifu husika tumeweza kusawiri mambo muhimu yanayoibuka kiradidi katika jamii za Kiafrika. Mfano kukosekana kwa haki, utawala wa mabavu, rushwa, kujilimbikizia mali, sihiri, ushujaa na kifo. Hivyo, kipengele hiki ni muhimu sana katika kazi za kisanaa ili kusisitiza dhamira zinazoibuka. Kutokana na matokeo ya kukichunguza kipengele hiki cha utokeaji wa motifu hasa motifu ya unguli, sihiri, kifo, kifungo, safari na msako katika kazi teule, tumegundua kuwa vipengele hivi vinatumiwa sana katika tamthiliya. Hivyo tunapendekeza kuwa

wasanii wajitokeze na kuandika kazi nyingi za kisanaa zenye kukisawiri vema kipengele hiki hasa kupitia kazi za tamthiliya na kutafiti zaidi.

MAREJELEO

Aristotle, M. (1958). *On Poetry & Style* (Mh. G.M.A Grube) New York: The bobs Merri co. me Indiana Polis.

BAKIZA (2008). *Utamaduni wa Mzanzibari*. BAKIZA.

Belcher, S. (1999). *Epic Traditions of Africa*. Bloomington, Indiana University Press.

Browning, A., & Elmes, M. R. (2015). *Lenses: Perspectives on Literature* (2nd ed). United State of America. Hayden - MCNeil Publishing.

Campbell, J. (1968). *The Hero with a Thousand Faces*. New York: Princeton.

Coser, L. (1963). *Sociology Throgh Literature: An Introductory Reader*. Englewood.

.

Johnson, J. W. (1982). “ On the Age and Other Primitive Thesis” In Zygas, E. V., and Voorheis, P. *Folkloical: Festchrift for Felix Oinas*, I. U. Press Bloomington.

Johnson, J. W. (1992). *The Epic of Son-Jara: A West Africa Tradition*. USA: Indiana University Press.

- Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers Limited.
- Kothari, C. R. (1992). *Research Methodology and Techniques*. New Delhi, Wiley Eastern Limited.
- Kunene, D. P. (1971). *Heroic Poetry of the Basotho*. Oxford: Oxford University Press.
- Kunene, D. P. (1985). "Journey as Metaphor in African Literature" Stephen Anold, ed African Literature Studies: The Present State/ L'et al Present Washton Three Continents Press.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.
- Marx, K. (1859). *A Contribution to the Critique of Political Economy*. New York: International Publishers.
- Mbele, J. L. (1986). *The Hero in the African Epic*. Ph. D Thesis. Madson: University of Winscosis.
- Mbiti, J. S. (2011). *African Religion & Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mbogo, E. (2008). *Ngoma ya Ng'wanamalundi*: Dar Es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers
- Mbogo, E. (2009). *Fumo Liyongo*. Dar es Salaam: Dar esSalaam University Press.
- Mbogo, E. (2011). *Sundiata* Dar es Salaam: TUKI.
- Mbogo, E. (2015). *Wangari Maathai*. Dar es Salaam: Vision Strategic

Impact Limited.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Dar es Salaam: East African Education.

Mlacha, S. A. K., & Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es salaam: Dar es Salaam University Press.

Mohamed, S. A. (2002). *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*: Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthiliya, na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, S. A. (1988). *Kiza Katika Nuru*. Nairobi, Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (1990). *Kivuli Kinaishi*, Nairobi: Oxford University Press.

Muhando, P. (1975). *Pambo*. Dar es Salaam: Swala Publications.

Mulokozi, M. M. (1986). *The Nanga Epoc of the Bahaya: A Case Study in African Epic Characteristics*. Ph.D Thesis, University of Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili: OSW 105*. Dar es salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, M. M. (2002). *The African Epic Controversy: historical, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic*

Poetry and Performance. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

- Mulokozi, M. M. (2003). “Utafiti katika Fasihi Simulizi” katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*. TUKI: Dar Es Salaam.
- Mutiso, T. (2012). “ Motifu ya Hirizi Katika Ushairi wa Kiislamu wa Kiswahili” . *Mulika Na. 31*: Dar es Salaam. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Narizvi, S. (1982). *The Sociology of Literature of Politics*. Australia: Edmund Burke.
- Niane, D. T. (2005). *Sundiata an Epic of Old Mali*. Translated by G.D. Pickett. England: Longman.
- Njogu, K., & Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mgogo, Y.P. (2017). Kuchunguza Hadithi za Wanyiha Katika Kurithisha Elimu ya Jadi. Tasinifu iliyowasilishwa kwa ajili ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Da es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mwangosi, G. (2018). Kuchunguza Dhamira na Fani Katika Nyimbo za Magosi za Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mwangoka, N. (2011). Motifu za Safari na Msako katika Makuzi ya Wahusika wa Riwaya za Kezilahabi. Tasinifu iliyowasilishwa kwa ajili ya shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Dar es

Salaam. Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Island: Augstan College Rock.

Nyamsenda, J. C. (2015). "Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Safari na Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari" Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (PhD). Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Okpewho, I. (1975). *The Epic in Africa: Towrd a Poetic of the oral Performance*. New York: Columbia University Press.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadhalia ya Fasihi Linganishi*. Karljamer Print Technology, Dar es Salaam, Tanzania.

Raymond, W. (1966). *Modern Tragedy*. London: Chatto & Windus

Robert, S. (1982). *Adili na Nduguze*. Dar es Salaam: Tanzania Publishinh House.

Samwel, M. (2013). *Tamthilia ya Kiswahili: Kutoka Miviga ya Kidini hadi Filamu*. Dar es Salaam: Meveli Publishers.

Sandars N. K (1960). *The Epic of Gilgamesh*. Cox & Wyman Ltd: Great Britain.

Selden, R. (1990). *The Theory of Criticism*. London: Macmillan.

Semzaba, E. (1997). *Tamthiliya ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publication Centre.

- Senkoro, F. E. M. K. (1997). "The significance of the Journey in Folk Tales From Zanzibar", *Tasinifu ya uzamivu (Hakijachapishwa) Chuo kikuu cha Dar es Salaam.*
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Senkoro, F. E. M. K. (1985). "Wahusika Katika Riwaya za Kiswahili Tanzania". (1970-1982), *MULIKA Na. 17*. Dar es Salaam: TUKI.
- Shemweta, D. (2015). Itikadi katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo. *Tasinifu ya shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*
- Shorter, A. (1969). *African Oral Tradition, History & Literature*. Columbia: Columbia University.
- Steiner, G. (1961), *The death of Tragedy*, London: Faber and Faber.
- Sungi, N. A. (2011). "Ruwaza ya shujaa Mwanamke wa Kiutendi katika jamii ya Wanyanyembe wa Tabora". (hajjachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Vogler C. (1998). "The Writer's Journey: Mythic Structure for Writers", 3rd ed. USA. Michael Wiese Production.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa tamthilia: historia na maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2000). "*Umatinishaji wa Historia ya Umatinishaji: Kaptula la Marx* (E. Kezilahabi). Dar es Salaam: TUKI.

- Wamitila, K. W. (1998). "A Philosophical Labyrinth: Tracing Two Critical Motifs in Kezirahabi's Prose Works". *Kyallo Wadi Wamitila Journal* AAP55: 79 - 91, http://www.swahili-literature.at/links/Swahili_sekunderliteratur.pdf, 15/06/2016 saa 12 jioni.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Publisher LTD.
- Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers Limited.
- Mortmer, M. (2006). "African Journey." *Research in African Literature*". Vol.22. no. 2 (1991): 169-174.<http://www.jstor.org/stable/3819831>(imesomwa:20-06-2018

Professionalizing Non- Formal Education to Uncover the Hidden Talents and Potentialities for the National Development of Tanzania

By

Noel Julius Ntawigaya

Teofilo Kisanji University-TEKU

Department of Education

P.o.Box 1104, Mbeya

noeljulius9@gmail.com

Abstract

This paper, intends to discuss the potential of non-formal education programmes to meet the challenges of learning needs, and uncovering of the hidden talents and potentialities for the out-of-school children, adolescents and adults to the National socio-economic development of Tanzania especially in this digital century. This paper examines the context of NFE programmes in Tanzania and its status of implementation. Through reviewing the related literatures, experiential from the context of Tanzania and using the documentary analysis as my study methods, this paper discusses the importance of NFE in developing the talents and potentialities of the out-of-school children, adolescent and adults. Moreover, this paper discussed the necessity of professionalizing NFE programmes and Non-formal educators as well as the challenges facing NFE. Since, NFE can provide relevant knowledge and skills, particularly for out-of-school children and unemployed youth and adults to promote social inclusion and development of the Nation, it is suggested that, there is a need of reformulating Non-formal education strategy to ensure its effective implementation as way of developing the talents and potentialities of this group of out-of-school children, adolescents and adults for the socio-economic developing of the country as formal education system.

Keywords: Formal education, Non-formal education, Out-of-school, Professionalization

Introduction

Living in the digital century needs high level of knowledge and literacy that reflects the advancement of science and technology. In this digital century, schooling is an agenda for one to develop his/her talents and potentialities for his/her survival all over the world. According to UIS (2013), it is increasingly recognized that school alone cannot provide quality basic education for 'all'. The global progress made towards

Education for All (EFA) since the World Education Forum in 2000 has arguably been significant, particularly with regard to enrolment and gender parity at primary level. Yet, there were more than 57 million out-of-school children of primary age worldwide in 2011. To mitigate the digital century's challenges which are in line with EFA goals which according to UNESCO (2002) aims at achieving universal primary education, particularly for girls, ethnic minorities and marginalized children and achieving a 50 per cent reduction in levels of adults illiteracy by 2015", the government of Tanzania has effectively started implementing free education policy by issuing a circular on how it would be executed effective from January 2016.

According to the Right to Education (2016), On November 27, 2015 the Tanzanian government issued Circular 5 which implements the Education and Training Policy 2014 and directs public bodies to ensure that secondary education is free for all children. This includes the removal of all forms of fees and contributions. The government Circular Number 5 of 2015 is part of implementation of the Education and Training Policy 2014 and realization of fifth phase President's pledge to provide free education to Tanzanian children. The directive revokes all other previous circulars that were providing for various parents' and guardians' contributions in public schools. The circular provides that the provision of free education means pupils or students will not pay any fee or other contributions that were being provided by parents or guardians before the release of new circular (Robi, 2016).

However, the government of Tanzania has been striving to ensure free formal education to achieve the sustainable Development Goal 4 as stated to its citizens especially children and youth, currently, there is no any government issued circular concurrently which aim at reforming Non-formal education programmes especially for the out-of-school group as an alternative strategy to ensure the achievement of Tanzania National Development Vision 2025, which according to URT (1999), this vision

2025, envisages Tanzania's transformation from its status as a least developed country to a middle income country whereby its pertinent aims to education include; the creation of a 'well-educated and learning society' and enjoyment of 'high quality livelihood'. This requires, universal primary education, the eradication of illiteracy, quality education, gender equality and the empowerment of women, the improvement of infrastructure with an emphasis on promoting science and technology education. Hence, illiteracy which incorporates those who dropped out of the school and those who never got the formal schooling opportunity with various reasons still not eradicated.

During the 50th International Literacy Day on 8th September, the Adult and Non-Formal Education Director, said, "the country's illiteracy rate has gone up by one per cent to reach 23per cent at the end of last year, figure increased from 77 per cent in 2012 to 78 per cent in 2015" (Tanzania Daily News, 2016). Also the number of children and young boys and girls, who drop schools for different reasons like pregnancies, family problems, fearing severe punishments from teachers and etc, is so high. For example in 2011 about 57085 primary school pupils which were 74.9% dropped out from school (URT, 2011). Dropping out from schools affect their education, and future employment and as well as the opportunity to reach their full potential in life. Therefore, the only way to help those who never went to school and those who missed the formal schooling opportunity as a result of dropping out and other reasons behind, it is to engage them in Non-formal education where they can opt for various programmes, so that they can continue developing their talents and their potentialities to cope with the digital century's life which needs not blinded mind in all spheres.

According to UNESCO (2016), from 2000 to 2015, the Millennium Development Goals tracked the efforts of Governments to achieve universal primary education and gender parity in education, and significant progress was made worldwide. With the adoption of the

Sustainable Development Goals and the Incheon Declaration: Education 2030: Towards inclusive and equitable quality education and lifelong learning for all, Governments expanded the scope of their goal to include universal secondary education and the progressive introduction of lifelong learning opportunities. Nevertheless, significant gaps remain. An estimated 61 million children of primary school age, 60 million children of lower secondary school age and 142 million children of upper secondary school age are out of the formal school system. This deficit is particularly acute in sub-Saharan Africa, where 29.8 million children remain out of school, nearly half all out-of-school children worldwide. Some 775 million adults, two thirds of them women, lack minimum literacy skills. In sub-Saharan Africa, 42 per cent of students drop out before graduating primary school; in South and West Asia, that figure is 33 per cent.

Coombs, Prosser, and Ahmed (1973) explain that, Non-Formal Education also includes non-institutionalized practices, which play an important role in lifelong learning practices, especially in developing countries. Also it was added by Van der Linden and Manuel, (2011) that, What is more, alternative education may integrate indigenous worldviews with the demands of global realities at the local level. Non-Formal Education has, therefore, the potential to meet the diverse educational needs of societies that are impeded or excluded from, or averse to, participating in formal education systems and institutional settings. Hence, it is true that young boys and girls who missed formal schooling in whatever reasons, have the great opportunity to develop and show their talents and potentialities through non-formal education in line to the global demands in their local area, even to excel up to the international level like those who benefited from formal schooling.

Evidence suggests, however, that improving adult literacy and numeracy levels as non-formal education programmes can help promote peace building and reconciliation (Okech, 2004). Hence, there is no doubt that,

failure to find the alternative to help them in developing their talents and their potentialities making them being not jobless people, it cannot only cost them by involving in various deviant behaviors and doing other evil deeds, but it can also cost their families as well as the entire society, because in one way or another they can be threats causing various violations and other dangerous social commitments especially in this digital century where survival depends on oneself creativity.

Therefore, it is in this context that, the thesis of this paper, intends to examine the potential of non-formal education programmes to meet learning needs, and uncovering of the hidden talents and potentialities for the out-of-school children and adolescents, basing on the country and regional reports and other existing literature to the National socio-economic development of Tanzania especially in this digital century.

The contextualization of non-formal education programmes in Tanzania

Understandings of Non-Formal Education by different stakeholders congregate around its juxtaposition against formal education. It is therefore noteworthy that understandings amongst organizations in Tanzania are not as broad as the UNESCO classification that encapsulates social and economic development programmes, (Macpherson 2007). NFE, as stated in the Primary Education Development Plan (GoT, 2001), is ‘education for out-of-school children and youth’ while according to the Adult Education/NFE Strategy (Got 2002a), it is ‘out of school education’.

The Adult and Non Formal Education Strategy (AE/NFES) of 2002, aims to ensure that, In partnership with the civil society, that out-of-school children, youth and adults have access to quality basic learning opportunities, especially girls, women, disadvantaged groups and nomads, with a view to improve the literacy level by 20%, and reducing the backlog of out-of-school children by mainstreaming at least the 11-13

year olds of the targeted groups; thus contributing to the creation of a lifelong learning society, improvement in people's livelihood, and to an increased awareness and prevention of HIV/AIDS (GoT, 2002b).

However, according to the objectives of AE/NFES as introduced in the year 2002, Tanzania has a good plan for the development of Adult and Non-formal education. Nevertheless, this strategy seem not to be practically implemented simply because, there is no any current reformation that has been done under this strategy with regard to the population increase which to a large extent, as long as the population increase, the number of out-of-school group which include children, adolescents and adults increase. It should be expected that, as long as various reformations take place to formal education system, should also take place to non-formal education simultaneously.

Being that a case, it's my opinion that, the AE/NFES is so much interesting as it reads though it is too old, but its implementation is poor because still yet Non-formal education programmes are not professionalized as well as Non-formal educators just as formal education system. Therefore, more desired efforts should be made by the government and other stakeholders to rework on this strategy to ensure its effective implementation for the betterment of this group of out-of-school children, adolescents and adults, as way of uncovering their hidden talents and potentialities especially in this digital century. Hence, in a summary point, I categorize Non-Formal Education programmes, that it should involve the following target populations in line to their characteristics:

